# Fuata Moyo Wako

## Inawezekana Kumjua
## Mungu Kibinafsi

John Gilchrist

08FollowYourHeart-Swahili-edited by SB.05.22.56pages.indd 1 27-05-2022 15:05:50

Kichwa cha asili cha kitabu:Follow your heart - Knowing God Personally is possible

© 2022, kwa Toleo la Kiswahili
Life Challenge
P.O. Box 50770-00200,
Nairobi, KENYA
**www.life-challenge.org**

Haki zote zimehifadhiwa. Hakuna sehemu ya kitabu hiki inayoruhusiwa kunakiliwa bila idhini ya maandishi, isipokuwa kwa nukuu fupi katika vitabu na mapitio.

Nukuu zote za Kurani zimetolewa kwenye: KURANI TAKATIFU, iliyofasiriwa na Sheikh Abdullah Saleh Farsi, chapa ya saba, 1993.

Nukuu za Biblia zimetolewa kwenye: NENO BIBLIA TAKATIFU, 2014.

Kimetafsiriwa na John Augustine Mabutagulwa, Zanzibar, Tanzania.

ISBN: 978-9966-895-43-1

Kimechapishwa nchini Kenya.

# Fuata Moyo wako

## Imani ya kweli au majukumu ya desturi za kidini?

Wakristo na Waislamu wana mambo mengi yanayofanana. Wanamwamini Mungu mmoja, wana sehemu takatifu za kuabudia (makanisa na misikiti), wana siku maalumu za kidini za kila mwaka (Krismasi, Ijumaa Kuu na Pasaka kwa Wakristo, Eid ul-Fitr, Eid ul-Adha, Laylatu'l Mir'aj na Laylatu'l Qadr kwa Waislamu), na hutenga siku moja kila wiki kwa ajili ya ibada ya jumuia ya waumini (Jumapili na Ijumaa mtawalia). Kwa nje dini hizo zinaweza kufanana sana. Ibada zao zinaweza kuwa rasmi na za mara kwa mara na za kujirudia. Hasa Sala ya Waislamu hufuata mfano ule ule kila siku, mwaka hadi mwaka, mwongo hadi mwongo bila ya kutofautiana. Adhan, yaani mwito wa sala, kamwe haubadiliki. Ibada ya hija hudumisha mwendelezo ule ule wa majukumu ya kidini ambayo yamekuwa yakitekelezwa kwa karne 14. Hakuna tofauti na makanisa mengi ya Kikristo. Padri wa Kikatoliki na Kiorthodox huimba sala zile zile zilizoamuriwa kama maimamu wa Kiislamu wanavyofanya.

Miaka kadhaa iliyopita mwanamke wa Kiislamu aliniambia, "Kila ninapokwenda makaburini huwa nikiyatazama makaburi yote ya Waislamu yaliyoko upande mmoja, na ya Wakristo upande mwingine, ninajiuliza 'Kuna tofauti gani?'" Sawa, kama unawatafuta walio hai katika waliokufa, haielekei kuonekana tofauti kubwa. Makundi yote matatu ya wale wanaomwabudu Mungu mmoja, ikiwa ni pamoja na dini ya Wayahudi, wameshikilia mifumo yao ya kidini kwa namna za kidesturi, wakirudia taratibu na sikukuu na siku takatifu zile zile



08FollowYourHeart-Swahili-edited by SB.05.22.56pages.indd 1 27-05-2022 15:05:50

kila mwaka, zote zikiwa na msingi wa mfanano wa nje na ibada ya kidesturi. Mwenye duka mmoja wa Kiislamu wa Yerusalemu alisema, "Biashara kubwa ni tatu pekee hapa Yerusalemu. Moja hukusanya hela siku za Ijumaa, ya pili siku za Jumamosi, na ya tatu siku za Jumapili."[1]

Kumwabudu Mungu mmoja kwa utaratibu uliozoeleka tu, je, hii ndiyo kweli anayoitaka Mungu? Kujitolea kiutumwa kwenye taratibu za kujirudia maisha yetu yote? Kuna mstari wa Biblia unaoonyesha jinsi hili linavyokosa maana. Nitayabainisha maneno makuu ya mstari ili kutusaidia kuliona jambo lenyewe hasa:

> *Kila kuhani husimama siku kwa siku akifanya huduma yake ya ibada, na kutoa tena na tena dhabihu zile zile ambazo haziwezi kamwe kuondoa dhambi.* (Waebrania 10:11)

**Tuna dini nyingi duniani. Hata hivyo mbingu huona zipo dini za aina tatu tu.**

Kinaya cha wazi ni pale unapolinganisha kurudia rudia huko na kushindwa kwake kufanikisha lo lote: kila - siku kwa siku - tena na tena - zile zile - na hata hivyo *haziwezi kamwe* kumfikisha mtendaji kwenye lengo!

Uislamu huweka mkazo mkubwa sana kwenye ibada ya kidesturi ya kila mara. Haipo nafasi ya mtu kuomba au kusifu mwenyewe kwa hiari wakati wa kutekeleza kila raka'ah. Mwislamu wa kweli hatakuwa tu na ndevu bali pia atazisawazisha zifikie urefu ulioamuriwa ili aifuate sunnah ya Muhammad. Ni lazima kuvaa kibaraghashia wakati wa sala msikitini. Lazima viatu viondolewe. Mienendo ile ile ya kuanza kwa kutawadha (wudhu) ni lazima ifuatwe wakati wote ili kutii amri ya Kurani: 'Osheni nyuso zenu na mikono yenu mpaka vifundoni, na mpake vichwa vyenu, na (osheni) miguu yenu mpaka vifundoni' (Surah

[1](Nukuu hii inatoka kwenye Discovery video - *Jerusalem: City of Heaven*)



08FollowYourHeart-Swahili-edited by SB.05.22.56pages.indd 2 27-05-2022 15:05:50

5:6). Kila ruku (kuinama) na sajdah (kusujudu) lazima kufanywe na wale wanaohudhuria kuabudu kwa pamoja bila kupishana, kwa namna ile ile, nyakati zile zile, kila siku. Kwenye kipindi cha qa'dah (namna ya kukaa) lazima taslim ile ile itamkwe kila muumini anapousalimia upande wake wa kushoto na wa kulia. Haliruhusiwi badiliko wakati wo wote kwenye utaratibu huu.

Uislamu hudai kwamba unatamka upya tu dini ya asili ya kunyenyekea kwa Mungu. Vile vile hudai kuwa manabii wote waliotangulia waliifuata. Kurani husema kuwa ilikuja tu kama tasdiq, yaani 'uthibitisho' wa yale yaliyotangulia (Surah 10:37), siyo namna mpya ya dini. Kama ni hivyo, dini ya kweli ya Mungu lazima wakati wote ililenga kwenye unyenyekevu wa kidesturi wa mara kwa mara, heshima ya mtumishi kwa Bwana aliye wa Kimungu, ambaye hawezi kujuliwa wala kupendwa kwa jinsi alivyo yeye binafsi.

Biblia ina picha tofauti kabisa. Haiioni dini ya Mungu kuwa vile vile wakati wote, ikifuata tu mifano ile ile ya ibada ambayo kamwe haijabadilika na haitabadilika. Kwa vile inavyojumuisha historia ya uhusiano wa Mungu na watu wake, huonyesha kukua na kupanuka kwa uhusiano huu anapozidi kuwakaribia walio wake, na humaliza kwa kilele chenye utukufu anapochukua jukumu la kuwakomboa watu wake na kuwakaribisha kwenye uhusiano na yeye mwenyewe ulio hai na wa mtu binafsi. Lazima utambue kuwa hao si watumwa waliolazimishwa kufanya maagizo, bali ni watoto waliozaliwa na Roho wake Mtakatifu, waliosamehewa dhambi zao, na walioandaliwa utukufu wa milele. Jiunge nami kwenye safari tunapougundua ujumbe wa Kikristo unaoonyeshwa kwenye maisha ya watumishi wa Mungu katika historia yote.



08FollowYourHeart-Swahili-edited by SB.05.22.56pages.indd 3 27-05-2022 15:05:50

## KAINI NA HABILI: DINI YA KWELI NA YA UONGO

Tuna dini nyingi duniani. Zinajumuisha dini ya Wayahudi iliyoanzishwa na Musa, Ukristo ulioanzishwa na Yesu, Uislamu ulioanzishwa na Muhammad, Ubuddha ulioanzishwa na Gautama Buddha, na nyingine nyingi kama Uhindu ambao waliouanzisha hawajulikani. Hata hivyo mbingu huona zipo dini za aina tatu tu. Ya kwanza ni kumkana Mungu, yaani kuabudu cho chote isipokuwa Mungu, kuabudu kiumbe badala ya Muumba. Kama ni kutukuza sanamu za kipagani, roho za wahenga au viumbe vingine, hakuna tofauti. Yote ni sawa kwa malaika wa mbinguni - kuabudu cho chote na kila kitu *isipokuwa* huyo Mungu wa kweli. Biblia huwaelezea kikamilifu wanaoabudu chochote na vitu vyote mbali na huyo Mungu wa kweli:

> *Kwa maana ingawa walimjua Mungu, hawakumtukuza yeye kama ndiye Mungu wala hawakumshukuru, bali fikira zao zimekuwa batili na mioyo yao ya ujinga ikatiwa giza. Ingawa walijidai kuwa wenye hekima, wakawa wajinga na kubadili utukufu wa Mungu aishiye milele kwa sanamu zilizofanywa zifanane na mwanadamu ambaye hufa, na mfano wa ndege, wanyama na viumbe vitambaavyo.*
>
> (Warumi 1:21-23)

Ufafanuzi unahitimisha:

> *... waliibadili kweli ya Mungu kuwa uongo, wakaabudu na kutumikia kiumbe badala ya Muumba, ahimidiwaye milele! Amen.* (Warumi 1:25)

### Dini Mbili za Zamani zaidi Duniani

Zaidi ya dini hiyo, zipo nyingine mbili tu, kama mbingu inavyoziona, na hizi ndizo za zamani zaidi kuwahi kuwako. Zilianzishwa siku ile ile na ndugu wawili, na kwa nje zinaweza kufanana sana. Ndugu hao walikuwa Kaini na Habili, wana wa



08FollowYourHeart-Swahili-edited by SB.05.22.56pages.indd 4 27-05-2022 15:05:50

Adamu na Hawa. Siku zilipofanyika sherehe za kwanza za kidini duniani, Kaini na Habili kila mmoja alileta matoleo kwa Mungu. Kaini alikuwa mkulima aliyeishi kwa mazao ya kutoka ardhini. Kwa hiyo alileta sehemu ya matunda ya jasho lake akamtolea Mungu. Lakini Habili alikuwa mchungaji wa kondoo, kwa hiyo alileta zawadi tofauti, sadaka ya wanakondoo wake na sehemu zao zenye mafuta. Ni kama haikuwako tofauti halisi kati ya hizo sadaka mbili, lakini Biblia inasema:

> ... *Bwana akamkubali Habili pamoja na sadaka yake, lakini Mungu hakumkubali Kaini pamoja na sadaka yake.*
> (Mwanzo 4:4-5)

Kilichofuata kinajulikana wazi: Kaini alikasirika akamwinukia ndugu yake na kumwua huko uwandani.

Kurani inathibitisha simulizi hiyo: "Na wasomee khabari za watoto wawili wa Adam kwa kweli. Walipotoa sadaka, Ikakubaliwa ya mmoja wao, na ya mwengine haikukubaliwa. Akasema (yule isiyokubaliwa sadaka yake): Nitakuua" (Surah 5:27). Hakuna kitabu kinachoelezea kwa nini sadaka ya Kaini ilikataliwa, lakini Biblia inaendelea kuonyesha kwa nini Habili alipata upendeleo kwa Mungu. Inasema:

> *Kwa imani Habili alimtolea Mungu dhabihu bora zaidi kuliko Kaini. Kwa imani alishuhudiwa kuwa mwenye haki, Mungu mwenyewe akazishuhudia sadaka zake. Kwa imani bado ananena ingawa amekufa.* (Waebrania 11:4)

Maneno makuu ni yale mawili ya mwanzo: kwa imani Habili alipata kibali cha Mungu.

**Imani ya Habili**

Sadaka ya Habili hudhihirisha imani hiyo ilivyokuwa. Aliwasilisha damu ya wanakondoo wake iliyomwagika. Habili alimpenda Bwana, lakini alitambua kwa uchungu kuwa nyakati fulani angeweza kuwa baridi kwa Mungu kama alivyokuwa Kaini kaka yake. Alijua alikuwa amehusishwa kwenye dhambi ya

wazazi wake katika bustani ya Edeni na kuwa hangeweza kutoa cho chote kwa Mungu kutokana na matunda ya juhudi zake mwenyewe ili ajikomboe. Lakini alijua vile vile kuwa Mungu alimwonya shetani bustanini:

*"Nami nitaweka uadui kati yako na huyo mwanamke, na kati ya uzao wako na wake, yeye atakuponda kichwa, nawe utamuuma kisigino."* (Mwanzo 3:15)

Kauli hii ya wazi ndiyo iliyokuwa tumaini la Habili. Siku moja Mungu atainua Mwokozi wa uzao wa Hawa, naye atateseka sana ili aulete wokovu wa wanadamu, lakini wakati huo huo atampa shetani jeraha la kufisha huku akiukomboa uzao wa Hawa kutoka kwenye nguvu za shetani. Hivyo sadaka ya Habili ilituma ujumbe wake yenyewe: "Ninaijua hali yangu ya dhambi na kuwa kwa njia za kidini siwezi kujitukuza kwako, lakini ninarudisha kwako kitu ambacho ni chako mwenyewe, kilichochinjwa na damu yake ikiwa imemwagika, kwa sababu ninahisi kukombolewa kwangu kutakuja kwa gharama kubwa kwako." Habili alikuwa mwanadamu wa kwanza kutoa imani ya kweli kwa Mungu. Kwa mtazamo wa mbingu, hii ndiyo dini ya pili iliyopo duniani, nayo ndiyo dini pekee ya kweli. Ni imani ya Habili.

**Dini ya Kaini**

Hata hivyo Kaini hakuwa na upendo wa kweli kwa Mungu. Katika kiburi chake na kujihesabia haki hakuamini kuwa anahusika katika dhambi ya wazazi wake. Pia alimkosoa Mungu akimchokoza:

*"... je, mimi ni mlinzi wa ndugu yangu?"* (Mwanzo 4:9)

Mara tu baada ya kumuua ndugu yake Habili kikatili. Hata hivyo Kaini alikuwa tayari kumtambua Mungu kuwa ni Muumba wake, kwa kuleta zawadi kama Habili, lakini zawadi yake ilikuwa ishara ya kazi yake tu, akitoa kutoka kwenye wingi alio nao kutokana na jasho lake. Huenda nyakati fulani alipenda



08FollowYourHeart-Swahili-edited by SB.05.22.56pages.indd 6 27-05-2022 15:05:50

kumwabudu Mungu, lakini aliyaona maisha yake mwenyewe na aliamini kuwa yuko huru kuitumia ardhi kwa faida yake mwenyewe tu. Huenda alikuja nyakati fulani kumsalimu Mungu, labda mara moja kwa wiki au kwenye sikukuu ya mavuno mara moja kwa mwaka, lakini si zaidi. Kaini alikuwa mwanzilishi wa dini ya kuabudu Mungu mmoja *kidesturi*, akimwabudu Mungu bila ya kuwa na upendo wa kweli kwake. Hii ndiyo Dini ya Kaini. Kwa mtazamo wa mbingu, hii ni dini ya tatu iliyopo duniani, nayo ni ya uongo kabisa. Ndiyo kubwa zaidi duniani siku hizi. Inakumbatia kila dalili ya kumwabudu Mungu mmoja kidesturi, na inaweza kuwa ya Kiyahudi, Kikristo au Kiislamu. Mungu mwenyewe aliijumuisha katika maneno haya:

> *"Watu hawa hunikaribia kwa vinywa vyao na kuniheshimu kwa midomo yao, lakini mioyo yao iko mbali nami. Ibada yao kwangu inatokana na maagizo waliyofundishwa na wanadamu."* (Isaya 29:13)

Hasira ya Kaini iliionyesha tofauti kati ya yeye na ndugu yake. Labda hata alijibu vikali: "Nilikuwa tayari kuja mara nyingi kukusalimu, hata mara moja kwa wiki ikihitajika. Kwa nini uliikataa kabisa sadaka yangu?" Labda jibu la Mungu kwake lilikuwa: "Habili alitoa sadaka moja tu, lakini ilikuwa ya kuyatoa maisha yake yote kwangu, akinitumaini kwa wokovu wake. Siku moja, *kwa sababu kwa dhabihu moja amewafanya kuwa wakamilifu milele wale wote wanaotakaswa.*" (taz. Waebrania 10:14). Imani ya Habili ndiyo dini pekee ya kweli ambayo ulimwengu umewahi kuitambua, na haitatokea nyingine. Ni imani hai inayosisimua ukilinganisha na ukavu wa kujifananisha kwa nje. Yenyewe haimpi Mungu cho chote, bali humtumaini Mungu pekee kwa wokovu wake. Haiangalii mwonekano wa nje na kusema, Mimi naonekana ni nani? Mwislamu, Myahudi, au Mkristo ninayetambuliwa kwa vazi, sharubu, baraghashia, majoho, kuhudhuria ibada kila wiki n.k., mambo yanayoonyesha utii wangu kwenye dini fulani? Hapana. Huuliza



08FollowYourHeart-Swahili-edited by SB.05.22.56pages.indd 7 27-05-2022 15:05:50

swali lisilofurahisha, Mimi yu nani? Ninampenda Mungu kwa kiasi gani nafsini mwangu, na nina utayari kiasi gani wa kuutafuta uaminifu wake, utakatifu na upendo wake, na haki yake, jinsi alivyo katika ukamilifu wake? Nikiondoa vazi la kidini, au sharubu, au majoho yangu ya kipadre, nitabaki ni nani? Nina nini *ndani* yangu cha kunipa sifa kwa Mungu? Kuna dini moja tu ya kweli duniani - ni ile imani ya mwanadamu inayoitikia au kutokea kama jibu kwa uaminifu wa Mungu. Hiyo ni mada tutakayoichunguza kikamilifu zaidi tunapoendelea.



08FollowYourHeart-Swahili-edited by SB.05.22.56pages.indd 8 27-05-2022 15:05:50

## IBRAHIMU:
## BABA WA WENYE IMANI

Waislamu wote wanamheshimu Ibrahimu kwa kusema ‘alayhis-salam’. Anatambuliwa kama mmoja wa mitume wakuu wa Mungu. Na Wakristo humwona kama mfano wa muumini wa kweli na baba wa wenye imani. Aliifuata imani ya kweli, imani ya Habili, na Wakristo wa kweli ni *wale walio wa imani ya Ibrahimu. Yeye ndiye baba yetu sisi sote.* (Warumi 4:16). Na Kurani huizungumzia “millata abikum Ibrahim”, “imani ya baba yetu Ibrahimu” (Surah 22:78). Lakini kwa nini Ibrahimu anajulikana kwa Mungu kwa imani yake na si kwa unyenyekevu wake wa kidini?

### Zaidi ya Unyenyekevu

Kurani huiona ‘millah’ ya Ibrahimu kama tu unyenyekevu usio na uhuru kwenye mapenzi ya Mwenyezi Mungu. Husema kuwa alikuwa mmoja wa ‘musliman’, yaani “aliyenyenyekea” (Surah 3:67) na hunena kuwa ‘Mola wake alipomwambia’: “Nyenyekea”; akanena: “Nimenyenyekea kwa Mola wa walimwengu (wote)” (Surah 2:131). Amri yenye maana ya “nyenyekea” kwenye andiko hili ni ‘Aslim’! na mwitikio wake ni aslamtu, “nimenyenyekea.” Maneno yote matatu hutoka kwenye herufi zile zile za msingi kama ‘uislamu’ na ‘mwislamu’. Hata hivyo hii siyo imani ya kweli. Ni kukubali tu mapenzi ya Mungu bila kupinga. Haizingatii imani ya nabii huyo katika uaminifu wa Mungu.

Biblia huonyesha kuwa Mungu alimwita Ibrahimu wajenge wenye kina zaidi kuliko tu kunyenyekea kwenye mapenzi yake. Uhusiano huu unaanza na ahadi aliyompa, Ibrahimu alipolalamika kuwa hana mrithi:

> *“Tazama juu kuelekea mbinguni na uhesabu nyota, kama hakika utaweza kuzihesabu.” Ndipo akamwambia, “Hivyo ndivyo uzao wako utakavyokuwa.”* (Mwanzo 15:5)



08FollowYourHeart-Swahili-edited by SB.05.22.56pages.indd 9 27-05-2022 15:05:50

**Kilikuwa kitu bora zaidi ambacho mtu ye yote angeweza kumpa Mungu.**

Linalofuata limeelezwa kwa urahisi huo huo:

*... akamwamini Bwana, naye kwake hili likahesabiwa kuwa haki.* Mwanzo 15:6)

Inaonekana kuwa rahisi mno – Ibrahimu aliichukua tu ahadi bila ya kuangalia undani wake, na kwa sababu alimwamini Mungu, alihesabiwa kuwa ni mwenye haki mbele zake. Hakulazimika kusali mara nyingi kwa siku, kufunga kwa miezi mingi, kwenda hija au kuwachangia maskini fedha nyingi ili akubaliwe na Mungu. Aliiamini tu ahadi na hapo hapo akawekewa mapatano na Mungu.

Hata hivyo imani yake ilijaribiwa mara kadhaa. Ilipita miaka mingi bila ya kutokea jambo lo lote. Mke wake, Sarai, ambaye hakuweza kuzaa watoto na alikuwa akizeeka, alimwambia Ibrahimu asaidie kwenye ahadi ya Mungu ya kupata uzao kupitia kwa mjakazi wake, Hagari (taz. Mwanzo 16:2). Alipozaliwa Ishmaeli, Ibrahimu alishawishika kuona kuwa huyo ndiye mrithi aliyeahidiwa. Lakini hatimaye, miaka 13 baadaye Ibrahimu alipokuwa na miaka 99 na mke wake akiwa na miaka 90 na bado hana mtoto, Mungu alimwambia:

*"Nitambariki na hakika nitakupatia mwana kwake. Nitambariki na kwamba atakuwa mama wa mataifa, wafalme wa mataifa watatoka kwake."* (Mwanzo 17:16)

Mwanzoni Ibrahimu aliyacheka matarajio hayo, lakini baadaye alitambua kuwa Ishmaeli hakuwa yule mwana wa ahadi ya Mungu.

*Ibrahimu akamwambia Mungu, "Laiti Ishmaeli naye angeshiriki baraka yako!" Ndipo Mungu akasema, "Ndiyo, lakini mkeo Sarai atakuzalia wewe mwana, nawe utamwita jina lake Isaka. Nitalithibitisha Agano langu naye kama Agano la milele kwa ajili yake na wazao wake baada yake.*

(Mwanzo 17:18-19)



08FollowYourHeart-Swahili-edited by SB.05.22.56pages.indd 10 27-05-2022 15:05:50

Hatimaye alipozaliwa Isaka, Sara alitaka Ibrahimu awafukuze Hajiri na Ishmaeli. Baba huyo akatatizwa sana, lakini Mungu alilithibitisha ombi la Sarai, na wakati huo huo alimtia moyo Ibrahimu kuwa atamfanya Ishmaeli naye awe taifa kubwa. Hata hivyo Ibrahimu alijaribiwa vikali wakati akitambua kuwa Ishmaeli amekataliwa na Mungu. Ishmaeli alifukuzwa alipokuwa na miaka 14 akawa anaishi jangwani.

**Jaribu kuu la Mwisho**

Kila Ibrahimu alipomtazama kijana wake mpya angalau alijua hakika kuwa ndiye mwana aliyeahidiwa. Aliitarajia siku ambapo Isaka atasimama kama utimilifu wa ahadi ya Mungu kwamba yeye atakuwa baba wa mataifa mengi. Lakini Isaka alipofikia umri aliofikia Ishmaeli alipofukuzwa, hatimaye Mungu alimwambia Ibrahimu tena. *"Ibrahimu!"* Mungu alimwita ghafula (Mwanzo 22:1). Ibrahimu aliitikia bila kusita, akitarajia kumsikia Mungu afafanue jinsi sasa mwanawe atakavyokuwa baraka kwa vizazi vijavyo. Badala yake, Mungu alimwambia:

> *"Umchukue mwanao, mwana wako wa pekee, Isaki umpendaye, uende katika nchi ya Moria. Mtoe huko kama sadaka ya kuteketezwa juu ya mlima mmojawapo nitakaokuambia."* (Mwanzo 22:2)

(Kurani pia inalo tukio hilo, lakini haitaji jina wala kutambulisha mwana aliyepangiwa kutolewa sadaka - Surah 37:102. Hata hivyo inathibitisha kuwa mfuatano wa 'nubuwwah' - unabii, na kitab – maandiko, ungefuata kwa kupitia uzao wa Isaka – Surah 29:27).

Hili lilikuwa jaribu kubwa zaidi kwa baba huyo. Ishmaeli alipoanza kuwa kijana, Mungu alimwagiza Ibrahimu amkatae, lakini sasa Isaka alipofikia umri ule ule katika maisha yake, Mungu alimwambia Ibrahimu amchinje! Lilikuwa jaribu kuu la upendo wa mwanadamu kwa Mungu – kumtoa mwanawe sadaka. Kama angemwachilia Mungu mwanawe, hakika



08FollowYourHeart-Swahili-edited by SB.05.22.56pages.indd 11 27-05-2022 15:05:50

Ibrahimu angempa Mungu vyote alivyokuwa navyo (linganisha na Warumi 8:32). Kilikuwa kitu bora zaidi ambacho mtu ye yote angeweza kumtolea Mungu.

Lakini Ibrahimu alikuwa akikabiliana na jaribu gumu zaidi. Mungu alimwahidi uzao mwingi kama nyota za angani kupitia mwanawe Isaka. Ahadi hii ingewezaje kutimia ikiwa atalazimika kumtoa mwanawe awe sadaka ya kuteketezwa? Ni lazima Ibrahimu alilifikiria tukio hili jinsi litakavyoonekana kwa macho. Kwanza picha imemtokea ya mwanawe akiwa majivu baada ya kutolewa sadaka na kuteketezwa. Kisha picha nyingine imemtokea ya upepo kuja na kupeperushia mbali majivu, na ameona jinsi yeye mwenyewe atakavyokata tamaa akisema, "Sasa ahadi ya Mungu inapeperushwa na upepo."

**Mungu anamsikiliza Mtumishi Wake**

Sasa, wakati huu Ibrahimu alikuwa ameshakua katika uhusiano wake na Mungu ya kunyenyekea tu kwenye mapenzi ya Mungu bila ya kuuliza maswali. Kwenye tukio jingine kabla ya hili, Mungu alipotishia kuiteketeza miji ya Sodoma na Gomora kwa uovu wao, Ibrahimu alihoji:

> *"Je, utawaangamiza wenye haki na waovu? Je, ikiwa watakuwepo watu wenye haki hamsini katika mji huo, hivi kweli utauangamiza na wala hutauacha kwa ajili ya hao watu hamsini wenye haki waliomo ndani yake? Hilo na liwe mbali nawe, kufanya jambo kama hilo, kuwaua wenye haki pamoja na waovu, kuwatendea wenye haki sawasawa na waovu. Iwe mbali nawe! Je, Mwamuzi wa dunia yote hatafanya lililo sawa?"* (Mwanzo 18:23-25)

Angewezaje nabii kuhoji maagizo ya Mungu? Huu haukuwa unyenyekevu. Lakini Mungu aliheshimu alivyofanya Ibrahimu, hatimaye akaahidi kutoiharibu miji hiyo hata kama wakipatikana humo wenye haki kumi tu. (Wala hawakufika kumi, na hatimaye ni Loti na binti zake wawili tu ndio waliookolewa kwenye uharibifu huo.)



08FollowYourHeart-Swahili-edited by SB.05.22.56pages.indd 12 27-05-2022 15:05:50

Hapa kuna mengi yaliyojificha. Ibrahimu alimtaka Mungu awe mwaminifu. Akiamini kuwa Mungu ni mwaminifu, aliiweka imani yake yote kwenye uaminifu wa Mungu. Ndiyo maana alipinga aliposikia jambo lililoonekana kana kwamba linausaliti uaminifu huo. Maandiko yanatamka kuwa *Kila neno la Mungu ni kamilifu* (Mithali 30:5), na Ibrahimu alikabiliana na agizo la kumtoa mwanawe sadaka lililomweka kwenye mtanziko wa aina hiyo hiyo. Ahadi ya Mungu ingewezaje kutimia kama Ibrahimu angemtoa sadaka Isaka? Ibrahimu alikuwa na nafasi ya kusema moyoni, "Mimi sijui, lakini si kitu. Mungu ameniagiza nimharibu Isaka, kwa hiyo nitafanya hivyo. Nitanyenyekea kwenye mapenzi yake bila kupinga. Ahadi isipotimia litakuwa tatizo lake, siyo langu."

**Kuakisi Uaminifu wa Mungu**

Lakini Ibrahimu hakufanya hivyo. Alijua kuwa imani yake, iliyompatia tamko la kuwa mwenye haki mbele za Mungu, ilikuwa mwonyekano tu wa uaminifu wa Mungu. Jua huleta nuru inayong'aa. Mwezi hauwezi ila kuiakisi kidogo tu nuru hiyo, lakini kama ukilikabili jua uso kwa uso, huiakisi kikamilifu. Ukiuondoa mwezi nuru ya jua inayong'aa itaendelea kudhihirika kikamilifu, lakini ukiliondoa jua mwezi hautaangaza hata kidogo. Hivyo Mungu huleta uaminifu kama jua linavyoleta nuru, lakini imani ya Ibrahimu ilikuwa kama nuru ya mwezi – kama kitu kinachouakisi tu uaminifu wa Mungu wenye utukufu.

> Ukiliondoa jua mwezi hauwezi kuangaza hata kidogo.

Hata hivyo Ibrahimu aliishikilia imani hiyo. Kama Habili, Ibrahimu naye aliendelea kuifuata dini pekee ya kweli duniani: *imani ya kweli*, na kama Habili alisifiwa kwa hilo:

*Kwa imani Ibrahimu, alipojaribiwa na Mungu, alimtoa Isaka kuwa dhabihu. Yeye aliyekuwa amezipokea ahadi za Mungu alikuwa tayari kumtoa mwanawe, aliyekuwa*



08FollowYourHeart-Swahili-edited by SB.05.22.56pages.indd 13 27-05-2022 15:05:50

*mwanawe pekee awe dhabihu. Ingawa Mungu alikuwa amemwambia Ibrahimu, "Uzao wako utahesabiwa kupitia kwa Isaka," Ibrahimu alihesabu kuwa Mungu angaliweza kumfufua Isaki kutoka kwa wafu. Na kwa kusema kwa mfano, alimpata tena Isaka kutoka kwa wafu.*

(Waebrania 11:17-19)

**Rafiki wa Mungu**

Mungu alimheshimu Ibrahimu na akamrudishia mwanawe. Ibrahimu alikuwa amelishinda jaribu la mwisho. Alikuwa tayari kumrudishia Mungu baraka iliyo kuu katika maisha yake, mwanawe wa kweli pekee, na katika hili aliikamilisha imani yake, akiamini kuwa pamoja na kumtoa Isaka kuwa sadaka, bado Mungu ataitimiza ahadi yake kwake kwa kumfufua mwanawe awe hai. Kwa hili Ibrahimu alipokea sifa maalum sana. Aliitwa rafiki wa Mungu. Karne nyingi baadaye, Yehoshafati mfalme mwenye haki wa Yuda, alimwomba Mungu:

*"Je, si wewe, Ee Mungu wetu, uliyewafukuza wenyeji wa nchi hii mbele ya watu wako Israeli, ukawapa wazao wa Abrahamu, rafiki yako, hata milele?"*

(2 Mambo ya Nyakati 20:7)

Mungu mwenyewe aliwahi kulizungumzia taifa la Israeli kuwa ni *"wazao wa Ibrahimu, rafiki yangu"* (Isaya 41:8). Yakobo, mwanafunzi wa Yesu na ndugu yake wa damu, naye aliandika kuhusu imani ya Ibrahimu na kuongeza *akaitwa rafiki wa Mungu* (Yakobo 2:23).

Kurani huithibitisha sifa hii: 'Na Mwenyezi Mungu amemfanya Ibrahimu kuwa ni kipenzi chake' (Surah 4:125). Neno la Kiarabu hapa ni Khalilan, "rafiki", na kwa hiyo Ibrahimu amekuwa akijulikana wakati wote kama khalilullah, kipenzi cha Mungu, katika Uislamu. Hata hivyo Kurani haitoi maelezo kuhusu sifa hiyo.



08FollowYourHeart-Swahili-edited by SB.05.22.56pages.indd 14 27-05-2022 15:05:50

Ni tofauti kwenye Biblia. Hapo tunaweza kuona zaidi na zaidi kuhusu imani ya kweli ni nini hasa. Mungu anataka kuwa na uhusiano ulio hai na watu wake. Anatamani hili zaidi sana kuliko utii wa kulazimisha kwa taratibu za kidini, kanuni za sikukuu, kushika kwa kurudiarudia sala zilizoagizwa, nyakati za sala, nk. Hili litadhihirika zaidi tunapoendelea. Wakati huu tuangalie ishara ya kutambuliwa kwa Ibrahimu – *imani ya kweli*. Mungu hakumwonyesha haki yake kwa kutumia nguvu, akitarajia Ibrahimu aonyeshe haki na utii kikamilifu kwa kila atakaloagizwa. Mtu hata akiwa mshika dini au mcha Mungu au aliyejitolea kiasi gani, hawezi kulingana na haki ya Mungu iliyo kamilifu. Dhambi yake itamvutia chini tena na tena.

Mungu alichagua kuuonyesha uaminifu kwa Ibrahimu na alifurahia nabii huyo alipoupokea daima kwa imani, mpaka hatimaye akaikamilisha alipoagizwa kumtoa mwanawe awe sadaka. Hili ni eneo muhimu la kuzingatia tunapoendelea. Tutaona jinsi imani ya Ibrahimu ya kujitoa sadaka ilivyokuwa kivuli tu cha upendo wa Mungu wa kujitoa sadaka utakaofunuliwa. Hata hivyo wakati huu tukamwangalie mtangulizi mwingine maarufu anayefuata katika historia ya Israeli, Musa, na tuone jinsi mipango ya Mungu na makusudio yake kwa ajili ya watu yalivyozidi kupanuka na kukua.



08FollowYourHeart-Swahili-edited by SB.05.22.56pages.indd 15 27-05-2022 15:05:50

# MUSA:
# ALIYEMJUA MUNGU USO KWA USO

Miaka zaidi ya mia nne ilipita kabla ya Mungu kuwasiliana tena moja kwa moja na watu wake. Baada ya miaka arobaini ya mafanikio akiwa mwana mfalme katika nchi ya Misri, na miaka arobaini mingine akiwa katika jangwa la Sinai kama mkimbizi, ghafula Musa alijikuta akiwa uso kwa uso na Mungu wa Israeli. Mungu alimwita ili alikomboe taifa kutoka kwenye utawala wa Farao. Baada ya mfululizo wa mapigo ambayo hatimaye yaliuvunja mgongo wa ubishi wa Misri, Musa aliwaongoza watu kwenye jangwa hilo hilo wakielekea kwenye nchi ya ahadi ya Kanaani.

## Usiku wa mwisho nchini Misri

Tukio la mwisho la habari hii maarufu linahitaji kusimuliwa upya hapa. Farao hakusalimu amri mpaka malaika kutoka kwa Mungu alipowachinja wazaliwa wa kwanza wa kila familia nchini Misri usiku mmoja tu. Waisraeli waliotii agizo la Mungu la kutoa sadaka ya mwanakondoo wa pasaka, hao pekee waliachwa hai. Waliagizwa kila nyumba

> "... *kuipaka baadhi ya hiyo damu kwenye vizingiti na kwenye miimo yote miwili ya milango."* (Kutoka 12:22)

Kisha waliagizwa,

> *"Shikeni maagizo haya yawe kanuni ya kudumu kwenu na kwa ajili ya wazao wenu."* (Kutoka 12:24)

Kisha malaika wa kifo alipita juu ya kila nyumba yenye *hiyo damu*, akapita bila ya kuangamiza. Mwelekeo wa wazi ulikuwa ukifunuka, uhusiano wa Mungu na watu wake ulipokuwa ukiendelea. Habili aliitoa damu ya wana-kondoo wake kama sadaka ya upatanisho, akilenga kwenye sadaka kubwa zaidi. Ibrahimu alikuwa tayari kumtoa mwanawe Isaka kama ishara hiyo hiyo ya sadaka kubwa zaidi itakayofuata. Sasa watu wa Israeli waliagizwa kuipaka damu kwenye miimo ya milango,



08FollowYourHeart-Swahili-edited by SB.05.22.56pages.indd 16 27-05-2022 15:05:50

damu iliyomwagika ya wana-kondoo wao wa sadaka. Imani ya kweli ilianza kujieleza yenyewe. Tumaini la watu wote wa kweli wa Mungu, wanaotumaini kikamilifu katika neema yake na si udini wao, lilizidi kulenga kwenye damu ya Mwana-kondoo wa kweli wa Mungu itakayomwagika baadaye. Waumini wa kweli walilitafakari hili, na wakaweka imani yao kwenye neema ya Mungu inayokomboa itakayofunuliwa kikamilifu.

**Mungu anazungumza moja kwa moja**

Si muda mwingi baada ya Waisraeli kuondoka Misri, Mungu alimwagiza Musa:

*"Nenda kwa watu ukawaweke wakfu leo na kesho. Waambie wafue nguo zao na wawe tayari siku ya tatu, kwa sababu siku hiyo, Bwana atashuka juu ya mlima Sinai machoni pa watu wote."* (Kutoka 19:10-11)

Siku ya tatu watu walitetemeka huku uwepo wa Mungu ulipodhihirishwa kwenye mlima. Huko Mungu alizungumza moja kwa moja na taifa, akiwapa zile amri kumi ambazo baadaye zitakuwa msingi wa sheria ya maadili ya Wayahudi. Lilikuwa tukio la kipekee, ambalo Mungu alikuwa akiliandaa kwa muda wa karne.

Musa hakutembelewa na malaika kama mpatanishi kutoka mbinguni.

Musa hakutembelewa na malaika kama mpatanishi kutoka mbinguni. Mungu mwenyewe alimkaribia nabii huyo na taifa, akionyesha nia yake ya kujihusisha kwa karibu na watu wa Israeli kuanzia sasa. Ili afunue uwepo wake kati yao, Mungu alimwagiza Musa atengeneze sanduku likiwa na kiti cha rehema juu yake, akasema:

*"Hapo juu ya hicho kifuniko, kati ya hao makerubi wawili walioko juu ya hilo Sanduku la Ushuhuda, hapo ndipo nitakapokutana nawe na kukupa maagizo yangu kwa ajili ya Waisraeli."* (Kutoka 25:22)



08FollowYourHeart-Swahili-edited by SB.05.22.56pages.indd 17 27-05-2022 15:05:50

**Uthibitisho wa wazi**

Taifa lilikuwa na uthibitisho wa wazi kuwa Mungu mwenyewe alikuwako katikati yao. Kila alipoingia Musa kwenye hema alililoliandaa kama mahali patakatifu pa kukutania ambamo sanduku liliwekwa,

> *... nguzo ya wingu ingeshuka chini na kukaa kwenye ingilio, wakati Mungu akizungumza na Musa.* (Kutoka 33:9)

Watu walipoliona wingu, waliinuka na kuabudu. Simulizi inahitimisha:

> *BWANA angezungumza na Musa uso kwa uso, kama vile mtu azungumzavyo na rafiki yake.* (Kutoka 33:11)

Musa alizidiwa kwa kuona utayari wa Mungu wa kusema na yeye mwenyewe na watu wake kwa uso akidhihirisha uwepo wake katikati yao. Akamwambia Mungu:

> Mungu alikuwa akielekea mbali ng'ambo ya desturi za kidini.

> *"Mtu yeyote atajuaje kuwa mimi pamoja na watu wako tumepata kibali mbele zako, usipokwenda pamoja nasi? Ni nini kingine kitakachoweza kututofautisha mimi na watu wako miongoni mwa watu wengine wote walio katika uso wa dunia?"* (Kutoka 33:16)

Musa aliomba kwa ujasiri mwingi:

> *"Basi nionyeshe utukufu wako." Ndipo BWANA akasema, "Nitapitisha wema wangu wote mbele yako, nami nitalitangaza Jina langu, BWANA, mbele ya uso wako. Nitamrehemu yeye nimrehemuye, na pia nitamhurumia yeye nimhurumiaye."* (Kutoka 33:18-19)

Kwa heshima yote inabidi kusema kwamba hata kwenye hatua hii uwepo na wema wa Mungu uliofunuliwa unazidi jambo lo lote la kulinganisha katika Uislamu. Baadaye kutakuwa na ukaribu na ushirika, na neema na upendeleo mkubwa zaidi



08FollowYourHeart-Swahili-edited by SB.05.22.56pages.indd 18 27-05-2022 15:05:50

sana kati ya Mungu na walio wake mwenyewe, lakini hata kwenye hatua hii uhusiano kati ya Mungu na watu wake ulikuwa umeyazidi sana matarajio ya juu zaidi yanayoweza kutolewa na Uislamu. Mungu mwenyewe alionekana katikati yao. Lile wingu, lililokuwa uthibitisho maalumu wa uwepo wake, lilielea juu ya kiti cha rehema mchana, na kuangaza usiku. Lilipoondoka, taifa lilijua kuwa linapaswa kufuata ili liwe karibu na Mungu maana alikaa katikati ya watu wake.

**Kuakisi utukufu wa Mungu**

Musa aliposhuka kutoka Mlima Sinai akiwa na mbao mbili zenye amri kumi zilizoandikwa na Mungu mwenyewe, Musa *hakujua kuwa uso wake ulikuwa uking'aa, kwa sababu alikuwa amezungumza na BWANA* (Kutoka 34:29). Kila aliporudi kutoka kuzungumza na BWANA wana wa Israeli *waliona kuwa uso wake* [Musa] *unang'aa* (Kutoka 34:35). Kurani huuthibitisha uhusiano wa kipekee wa moja kwa moja kati ya Mungu na Musa: 'Na Mwenyezi Mungu akamsemeza Musa' (Surah 4:164). Haisemi zaidi, lakini inathibitisha uhusiano maalumu kati yao. Habari za Musa katika Biblia huhitimisha kwa maneno haya:

> *Tangu wakati huo, katika Israeli hajainuka nabii mwingine kama Musa, ambaye BWANA alimjua uso kwa uso.*
> (Kumbukumbu 34:10)

Ibrahimu aliitwa rafiki wa Mungu. Musa alisema na Mungu uso kwa uso kama mtu asemavyo na rafiki yake. Hapa tunaona ukuaji wa kusudi kuu la Mungu ukifunuliwa hatua kwa hatua. Uwepo wa Mungu ulidhihirika kwa ukaribu mno hata uso wa Musa ukang'aa aliposema naye. Mungu alikuwa akilenga zaidi sana kuliko tu mazingatio ya kidini. Nia yake hasa, kuwa watu wake wajieleze wao binafsi kwake na wamjue uso kwa uso, ilikuwa ikizidi kujifunua muda ulivyozidi kuendelea.



08FollowYourHeart-Swahili-edited by SB.05.22.56pages.indd 19 27-05-2022 15:05:50

### Migogoro na mapigano

Cha kuhuzunisha, ukaribu wa Mungu ulisababisha migogoro na mapigano kati yake na watu wa Israeli. Mara kwa mara walimtuhumu na kumwasi. Tangu mwanzo, Mungu alipolitaka taifa lisikie neno lake na kuzipokea amri zake kumi, watu walimwambia Musa:

*"Sema nasi wewe mwenyewe, nasi tutakusikiliza. Lakini usimwache Mungu aseme nasi, la sivyo tutakufa."*

(Kutoka 20:19)

Musa alipopanda mlimani akazungumze na Mungu kwa siku arobaini, watu waliinuka na kujaribu kumkataa Mungu asiwepo wala kuwatawala. Walitengeneza ndama wa dhahabu na kumwabudu, wakielekea papo hapo kuvunja kila agizo ili wamwambie wazi wazi walifikiri nini juu yake.

Hasira ya Mungu ikawa kubwa ndani yake. Mara nyingi alitishia kuwaharibu.

*Bwana akamwambia Musa, "Nimeona watu hawa, nao ni watu wenye shingo ngumu. Sasa niache ili hasira yangu ipate kuwaka dhidi yao, nami nipate kuwaangamiza."*

(Kutoka 32:9-10)

Alikuwepo Mungu mwema lakini mwenye haki katikati ya watu waovu na wakaidi – mgogoro ulikuwa usiozuilika. Taifa halikutaka kumkaribia Mungu. Kwa sababu ya kutoamini kwao aliwafanya wazurure jangwani kwa miaka arobaini wakiwa na kiasi kidogo kabisa cha chakula na maji. Pamoja na wema wote wa Mungu kwao, hawakumkaribia. Yeye akiishi karibu kabisa nao, ilikuwa ni lazima kwamba uovu na ugumu wa mioyo yao ulipingana vikali na haki yake na utakatifu wake.

### Kusudi kuu la Mungu

Musa aliwaambia Waisraeli:

*Na sasa, ee Israeli, Bwana Mungu wako anataka nini kwako ila kumcha Bwana Mungu wako, kwenda katika njia zake,*



08FollowYourHeart-Swahili-edited by SB.05.22.56pages.indd 20 27-05-2022 15:05:50

*kumpenda na kumtumikia Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote na kwa roho yako yote, na kuyashika maagizo ya Bwana na amri zake ninazokupa leo kwa mafanikio yako mwenyewe?* (Kumbukumbu 10:12-13)

Katika hili Musa alililifunua kusudi kuu la Mungu – uhusiano wa kina wa pande zote mbili uliojengwa kwenye msingi wa kupendana na utii wa watu kwa Mungu. Hata alipoweka namna mbalimbali za sheria na kanuni ili awavute siku zote kumfanyia ibada angalau ya kidesturi, walimkataa. Mioyo yao kabisa hawakutaka kumkaribia katika usafi na uaminifu na upendo. Hata walisema wangependa kurudia utumwa wao wa mwanzo huko Misri kuliko kuishi kwa imani katika uaminifu wa Mungu na kumruhusu Roho wake kuchunguza mioyo yao na nafsi zao.

Karne kadhaa baadaye Mungu alianza tena kuonyesha uwepo wake kati ya watu wa Israeli. Mtu mwingine aliinuka akiwa na upendo unaowaka kwa Mungu, mtu mwenye nguvu aliyeweza kuliunganisha taifa, na Mungu alimkaribia ili kusema naye, maana ilionekana matumaini yake kwa taifa yatazaa matunda.



08FollowYourHeart-Swahili-edited by SB.05.22.56pages.indd 21 27-05-2022 15:05:51

## DAUDI:
## MTU ANAYEUPENDEZA MOYO WA MUNGU

Daudi alipoanza kuwa mfalme wa Israeli, Mungu alisema:

*'Nimemwona Daudi mwana wa Yese, mtu anayeupendeza moyo wangu, atakayetimiza mapenzi yangu yote.'*

(Matendo 13:22)

Hakuwa akizungumzia udini wa Daudi, mwonekano wake wa nje, au jinsi yake ya kushikilia siku takatifu, bali alikuwa akizungumzia utu wake wa ndani – uadilifu wa roho yake, upendo wake kwa Mungu, tabia yake iliyofanywa upya, uaminifu wake na imani yake yenye kina. Daudi alionyesha kujikabidhi kwake kwa Mungu kwenye zaburi zake nyingi. Alikuwa mtu wa udhaifu mwingi, lakini pamoja na haya alimtamani Mungu na moyo wake ulimgeukia daima. Aliomba:

*Kama vile ayala aoneavyo shauku vijito vya maji, ndivyo nafsi yangu ikuoneavyo shauku, Ee Mungu. Nafsi yangu inamwonea Mungu kiu, Mungu aliye hai.* (Zaburi 42:1-2)

Kwenye wimbo wake mwingine wa sifa Daudi alitamka:

*Nakupenda wewe, Ee BWANA, nguvu yangu. BWANA ni mwamba wangu, ngome yangu na mwokozi wangu, Mungu wangu ni mwamba, ambaye kwake ninakimbilia. Yeye ni ngao yangu na pembe ya wokovu wangu, ngome yangu. Ninamwita BWANA anayestahili kusifiwa, nami ninaokolewa kutoka kwa adui zangu.* (Zaburi 18:1-3)

Hakuwa akikariri kitabu cha sala, alikuwa akionyesha imani yake ya kina kwa Mungu. Alijua kuwa imani ya kweli hutokana na kiini cha nafsi iliyomgeukia Mungu. Hakuonyesha mwonekano wa nje wa uadilifu kwenye ulimwengu unaomzunguka, huku akibaki bila ya kufanywa upya kwa ndani. Alitamani awe safi katika mawazo, maneno na matendo yake yote. Alitamka:



08FollowYourHeart-Swahili-edited by SB.05.22.56pages.indd 22 27-05-2022 15:05:51

*'Ee Mungu, nichunguze, uujue moyo wangu nijaribu na ujue mawazo yangu. Uone kama kuna njia iletayo machukizondani yangu, uniongoze katika njia ya milele.*
(Zaburi 139:23-24)

**Unyenyekevu wa kweli katika udhaifu**

Aliposhindwa aliuchunguza moyo wake na kuomba:

*Hakika wewe wapendezwa na kweli itokayo moyoni,ndani sana ya moyo wangu wanifundisha hekima.* (Zaburi 51:6)

Akaendelea:

*Ee Mungu, uniumbie moyo safi, uifanye upya roho ya uthabiti ndani yangu. Usinitupe kutoka mbele zako wala kuniondolea Roho wako Mtakatifu. Unirudishie tena furaha ya wokovu wako, unipe roho ya utii, ili initegemeze.*
(Zaburi 51:10-12)

Unyenyekevu wa kweli mbele za Mungu unatokea vile vile wakati anaendelea kuomba:

*Bali dhabihu za Mungu ni roho iliyovunjika, moyo uliovunjika wenye toba, Ee Mungu, hutaudharau.* (Zaburi 51:17)

Daudi aliteuliwa aiongoze Israeli kwa sababu moyoni mwake alikuwa mwaminifu kwa Mungu. Aliifahamu imani ya kweli. Alijua ni utayari wa kutafuta kufanywa upya kwa ndani, mwitikio kwenye uaminifu wa Mungu ulio thabiti. Mungu alipomwagiza Samweli kummiminia mafuta Daudi awe mfalme wa Israeli, alimwambia:

*"Bwana hatazami katika vile vitu mwanadamu avitazamavyo. Mwanadamu hutazama katika sura ya nje, lakini Bwana hutazama moyoni."* (1 Samweli 16:7)

Daudi alilijua na alilielewa hili.

Katika maisha yake yote Daudi alijitahidi kuliunganisha taifa la Israeli katika kumwabudu Mungu mmoja wa kweli. Alipoweza



08FollowYourHeart-Swahili-edited by SB.05.22.56pages.indd 23 27-05-2022 15:05:51

kupumzika baada ya kuwashinda maadui zake wote, Daudi alimwambia nabii Nathani:

*"Mimi hapa, ninaishi katika jumba la kifalme la mierezi, wakati Sanduku la Mungu limebaki katika hema." Nathani akamjibu mfalme, "Lolote ulilo nalo moyoni, endelea ukalifanye, kwa maana Bwana yu pamoja nawe."*

(2 Samweli 7:2-3)

"Mimi nitakuwa Baba yake na yeye atakuwa Mwanangu."

Daudi alipendekeza kumjengea Mungu hekalu zuri, awalete watu wa Israeli pamoja siku zote wakimwabudu Mungu mahali ulipo utukufu wake. Lakini Mungu alimwambia Nathani aongee na Daudi akisema:

*"Siku zako zitakapokwisha nawe ulale pamoja na baba zako, nitainua mzao wako aingie mahali pako, ambaye atatoka viunoni mwako, nami nitauimarisha ufalme wake. Yeye ndiye atakayejenga nyumba kwa ajili ya Jina langu, nami nitaimarisha kiti cha enzi cha ufalme wake milele. Nitakuwa baba yake, naye atakuwa mwanangu."*

(2 Samweli 7:12-14)

Mungu alimwambia Daudi kuwa mwanawe ndiye atakayelijenga hekalu alilopendekeza, na akahitimisha kwa kuahidi:

*"Nyumba yako na ufalme wako utadumu milele mbele zangu, kiti chako cha enzi kitafanywa imara milele."*

(2 Samuel 7:16)

## Mwana aliyeahidiwa

Kama Mungu alivyotoa ahadi ya mtoto kwa Ibrahimu, sasa alimwahidi na Daudi. Sulemani ndiye huyo mwana wa ahadi, na baada ya kifo cha baba yake alianza kulijenga hekalu la kwanza la Kiyahudi. Kwenye vizazi vilivyofuata watu wa Israeli walihisi kuwa, huku Sulemani akiwa mwana aliyeahidiwa wa wakati



08FollowYourHeart-Swahili-edited by SB.05.22.56pages.indd 24 27-05-2022 15:05:51

huo wa Daudi, unabii ulizungumzia pia mwana adhimu zaidi atakayekuja. Mungu alikuwa amemhakikishia Daudi kuwa huyo mwana wa ahadi atatawala juu ya ufalme wake milele. Mara baada ya Sulemani kufa, watu walitambua kuwa unabii utatimia kikamilifu tu atakapofika huyo Mwana wa Daudi aliye adhimu zaidi, na waliitazamia siku yake. Mungu alikuwa amemwambia wazi Daudi kuwa huyo Mwana ajaye aliye adhimu zaidi atakuwa Mwana wa Mungu *mwenyewe*. Mungu aliongezea ili kuondoa utata wo wote: *"Nitakuwa Baba yake, na yeye atakuwa mwanangu."*

Unabii huo unapatikana kwenye Maandiko ya Wayahudi (Agano la Kale), si andiko la Kikristo la baadaye. Kama Waislamu, Wayahudi nao kamwe hawajaamini kuwa Mungu ana Mwana, lakini hapa hapa, kwenye kitabu chao wenyewe (taz. 2 Samweli) kinachoheshimiwa na Wayahudi kuwa ni neno la Mungu kwa vizazi vyote tangu kilipoandikwa, ilitabiriwa wazi wazi katika ahadi ya Mungu kuwa Mwana wake mwenyewe atakuja ulimwenguni kuimarisha ufalme wake wa milele. Ahadi hiyo imethibitishwa kwenye kifungu kingine:

> *Naye ataniita kwa sauti, 'Wewe ni Baba yangu, Mungu wangu, Mwamba na Mwokozi wangu.' Nitamteua pia awe mzaliwa wangu wa kwanza, aliyetukuka kuliko wafalme wote wa dunia. Nitadumisha upendo wangu kwake milele, na agano langu naye litakuwa imara. Nitaudumisha uzao wake milele, kiti chake cha enzi kama mbingu zinavyodumu.*
> (Zaburi 89:26-29)

Nukuu hii nayo inatoka kwenye moja ya vitabu ambavyo ni kiini cha Maandiko ya Wayahudi, kilichoandikwa miaka elfu kabla ya Ukristo kuanza.

Ahadi zote mbili za kupata mwana, ile iliyotolewa kwa Ibrahimu na nyingine kwa Daudi, zilikuja ghafla bila kutanguliwa na tangazo wala tarajio lo lote. Ukiyasoma Maandiko ya Wayahudi utastaajabu jinsi unabii wote unavyoshtusha, maana



08FollowYourHeart-Swahili-edited by SB.05.22.56pages.indd 25 27-05-2022 15:05:51

kabla yake hakuna kinachodokeza lo lote la yajayo. Mungu alichagua tu muda mwafaka wa kuzungumzia mambo yajayo, huku makusudio yake kwa wanadamu na mipango yake kwa ajili ya ukombozi ikiendelea kujitokeza.

**Mungu alidhihirisha wazi uwepo wake**

Sulemani alipolikamilisha Hekalu na makuhani wakaja kutoka humo baada ya kuliweka sanduku la agano penye patakatifu pa patakatifu:

> *... wingu likajaza Hekalu la Bwana. Nao makuhani hawakuweza kufanya huduma yao kwa sababu ya lile wingu, kwa kuwa utukufu wa Bwana ulijaza Hekalu lake.*
>
> (1 Wafalme 8:10-11)

Kwa mara nyingine Mungu alidhihirisha wazi uwepo wake kwa taifa kama alivyofanya wakati Musa alipoikamilisha hema ya kukutania jangwani. Uislamu kamwe haujawa na cho chote cha kulinganisha na hili.

Kwenye miaka arobaini ya Waisraeli kuzunguka jangwani kwa sababu ya kutoamini kwao, taifa lilinyang'anywa mazingira yake yenye baraka wakapewa tu mana ya kula na maji ya kunywa. Watu waliteseka chini ya shinikizo hili Mungu alipowajaribu vikali aone kama watakuwa waaminifu kwake au la. Aliwaonyesha kwa nguvu haki yake, na kila walipokosa kumtii aliwaadhibu mara moja, akituma tauni na moto kwenye kambi zao.

**Amani na mafanikio yasiyo na kifani**

Hata hivyo sasa Mungu aliwapa Waisraeli miaka arobaini ya amani na mafanikio makubwa. Wakati huu aliiacha hali hii iendelee, akifurahi kwa kuwa agano alilofanya na Musa hatimaye lilionekana kufanya kazi. Matumaini yake kwa taifa yalikuwa yamefikia kilele na aliliruhusu lifurahie fahari yake. Hata maadui wa Israeli walikuwa na amani na watu wa Mungu. Ilikuwa enzi ya heri, na ishara ya amani na utukufu ujao wa mbinguni.



08FollowYourHeart-Swahili-edited by SB.05.22.56pages.indd 26 27-05-2022 15:05:51

*Mfalme akafanya fedha kuwa kitu cha kawaida kama mawe huko Yerusalemu, mierezi akaifanya kuwa mingi kama mikuyu vilimani.* (1 Wafalme 10:27)

**Matumaini yaliyoharibiwa**

Cha kusikitisha, 'fungate' kati ya Mungu na watu wake haikudumu muda mrefu. Sulemani alishindwa kulenga imani yake katika Mungu akageukia ubadilifu wa mwili. Alioa wake wa kigeni walioanzisha mila za kipagani kwenye taifa. *Solomoni akakaza kuwapenda* (1 Wafalme 11:2). Alipozeeka wake zake wa kigeni:

*... wakaugeuza moyo wake kuelekea miungu mingine, na moyo wake haukujitolea kikamilifu kwa Bwana Mungu wake, kama ulivyokuwa moyo wa Daudi baba yake.*

(1 Wafalme 11:4)

Alipokufa Sulemani taifa liligawika yakatokea mawili, watu wa Yuda wakimfuata Rehoboamu, mwana wa Sulemani, kama mfalme wao, huku makabila ya kaskazini ya Israeli yakimfuata Yeroboamu aliyeziweka ndama za dhahabu huko Dani na Betheli kuwavuruga watu wasimwabudu BWANA huko Yerusalemu. (Taz. 1 Wafalme 12:28-29)

Mungu akamwambia Yeroboamu:

*"Umefanya maovu mengi kuliko wote waliokutangulia. Umejitengenezea miungu mingine, sanamu za chuma, umenighadhibisha na kunitupa nyuma yako."*

(1 Wafalme 14:9)

> Alitafuta mbadala wa hukumu.

Mfuatano wa wafalme waovu uliyapeleka makabila ya Israeli kwenye kila namna ya ibada ya sanamu na uovu. Historia ya Yuda ilikuwa ya kupanda na kushuka – baadhi ya wafalme wake kama Ahazi walikuwa wabaya kama wafalme wa Israeli, huku wengine kama Yehoshafati waliwafanya watu kuwa waaminifu



08FollowYourHeart-Swahili-edited by SB.05.22.56pages.indd 27 27-05-2022 15:05:51

kwa Mungu. Lakini lilikuwa suala la muda tu kabla ya taifa la Yuda nalokurudi nyuma tena na kumkasirisha sana Mungu.

Matumaini ya Mungu kwa taifa yalikuwa yameharibiwa. Hasira yake ikawa kali dhidi yake. Angeweza mara moja kuwakusanya Israeli na mataifa yote ya dunia awahukumu, lakini hakufanya hivyo. Mungu wa uaminifu wote, ambaye upendo wake kwa watu wake ulikuwa upeo, kwa mkazo wenye hamaki chanya, alifikiria uwezekano wa kuwaleta tena watu wake kwenye uhusiano wa kibinafsi wenye kina kama alivyokusudia. Alitafuta mbadala wa hukumu. Afanyeje? Ahukumu au akomboe? Upendo wake wa kimungu ulimfanya achague la pili, lakini si baada ya kutafakari kwa undani sana ni gharama gani itakayobidi yeye mwenyewe kuilipa ili alikamilishe kusudi lake.



08FollowYourHeart-Swahili-edited by SB.05.22.56pages.indd 28 27-05-2022 15:05:51

## YEREMIA NA EZEKIELI: AHADI YA AGANO JIPYA

Hata vitabu 17 kati ya 39 vya Maandiko ya Wayahudi hutoka kwenye wakati wa manabii Yeremia na Ezekieli. Waliishi kama miaka mia tatu baada ya Sulemani na Daudi. Maandishi ya wakati huo, isipokuwa kitabu cha Yona, ni maandishi ya kinabii. Yamejaa unabii kuhusu yajayo na yanalenga ufunuo wa Mungu unaopanuka na kilele kile ambacho ufunuo huo unakielekea. Hata hivyo baadhi ya nukuu za vitabu hivi huonyesha tu hasira ya Mungu ilivyokuwa na kina juu ya watu wake sababu ya hawa kwa kuzidi kumkataa wakati huo.

### Hasira kali

Mungu alitamka,

*"Hasira yangu inawaka dhidi ya wachungaji, nami nitawaadhibu viongozi; ..."* (Zekaria 10:3)

Tena alisema:

*Ole wao, kwa sababu wamepotoka kutoka kwangu! Maangamizi ni yao kwa sababu wameniasi! Ninatamani kuwakomboa, lakini wanasema uongo dhidi yangu.*

(Hosea 7:13)

Tena alisema:

*"Kwa kuwa ninajua hesabu ya makosa yenu na ukubwa wa dhambi zenu. ... Ninachukia, ninazidharau sikukuu zenu za dini; siwezi kuvumilia makusanyiko yenu."*

(Amosi 5:12,21)

Hata hivyo haikuwa hasira kali tu iliyomsababisha Mungu kusema kwa nguvu vile, ilikuwa pia huzuni kubwa kwa sababu taifa alilolichagua na kulipenda kutoka kwenye kina cha nafsi yake limechagua kumkataa na kumweka pembeni, kama tunavyoona kwenye kifungu hiki:



08FollowYourHeart-Swahili-edited by SB.05.22.56pages.indd 29 27-05-2022 15:05:51

*"Nilipompata Israeli, ilikuwa kama kupata zabibu jangwani; nilipowaona baba zenu, ilikuwa kama kuona matunda ya kwanza katika mtini. Lakini walipofika Baal-Peori, walijiweka wakfu kwa ile sanamu ya aibu, nao wakawa najisi kama kitu kile walichokipenda.* (Hosea 9:10)

Kwa hiyo Mungu alitamka:

*"Kwa sababu ya uovu wao wote huko Gilgali, niliwachukia huko. Kwa sababu ya matendo yao ya dhambi, nitawafukuza katika nyumba yangu. Sitawapenda tena, viongozi wao wote ni waasi."* (Hosea 9:15)

**Upendo mkuu**

Lakini kati ya nukuu hizo, ambazo ni uteuzi tu kati ya matamko mengi ya hukumu, unakuja wingi wa vifungu kama hivyo kuhusu hasira yake ambapo Mungu anautamka upendo mkuu kwa watu wake na shauku yake kwa ajili ya kukombolewa kwao.

*"Nitaiimarisha nyumba ya Yuda na kuiokoa nyumba ya Yosefu. Nitawarejesha kwa sababu nina huruma juu yao. Watakuwa kama watu ambao sijawahi kuwakataa kwa sababu mimi ndimi Bwana Mungu wao, nami nitawajibu."* (Zekaria 10:6)

Tena alitamka:

*"Moyo wangu umegeuka ndani yangu, huruma zangu zote zimeamshwa. Sitatimiza hasira yangu kali, wala sitageuka na kumharibu Efraimu. Kwa kuwa mimi ndimi Mungu, wala si mwanadamu, Aliye Mtakatifu miongoni mwenu. Sitakuja kwa ghadhabu."* (Hosea 11:8-9)

Vifungu vingine vingi huonyesha jinsi mihemuko kutoka moyoni mwake ilivyokuwa na nguvu ndani yake. Aliwapenda watu wake, na huruma yake kwa ajili yao ilifikia upeo, lakini ghadhabu na hasira yake juu ya ubaridi wa mioyo yao nayo ilikuwa imefikia upeo wake.



08FollowYourHeart-Swahili-edited by SB.05.22.56pages.indd 30 27-05-2022 15:05:51

**Mioyo Iliyoasi**

Halikuwa suala tu la kurusha sarafu na kuchagua itakayoshinda. Kwenye Biblia yote tunaona kuwa msimamo wa Mungu kuhusu dhambi ni thabiti. Hazioni dhambi wanazofanya wanadamu kuwa ni kukosea tu au kushindwa tu kuamua jambo ipasavyo, hivyo zinaweza kusamehewa tu kwa urahisi. La! Ukweli ni kwamba hizo ni uasi na chukizo kwenye utakatifu wa Mungu. Tangu mwanzo Adamu na Hawa walipomwasi, Mungu ameuona uovu wa mwanadamu kuwa ni *tabia ya uasi*. Huonyesha kuwa wanadamu hawampendi Mungu, mioyo yao inamdharau, hawaujali uhusiano wa karibu na yeye ambapo Roho wake ana uhuru wa kuuchunguza utu wao wa ndani na kuzisafisha nafsi zao. Kushika nyakati za sala na kufunga zilizopangwa, mwonekano wa nje kimila, hayo yote hayawezi kuwa suluhisho kwenye moyo ulio na dharau kwake. Vile vile kuyatekeleza hayo yote si uthibitisho wa utii unaotoka moyoni.

Msimamo wa Mungu kuhusu dhambi ni thabiti.

Vitabu vilivyooandikwa kwenye hali hii nyeti ya historia ya Israeli huonyesha tu Mungu anavyojisikia kuhusu uovu wa wanadamu. Hapa kuna maoni yake ya msingi kuhusu hali ya wanadamu:

> *Moyo ni mdanganyifu kuliko vitu vyote, ni mwovu kupita kiasi. Ni nani awezaye kuujua? "Mimi Bwana huchunguza moyo na kuzijaribu nia, ili kumlipa mtu kwa kadiri ya mwenendo wake, kwa kadiri ya matendo yake yanavyostahili."* (Yeremia 17:9-10)

Nukuu nyingine mbili kutoka kwenye vitabu vilivyoandikwa wakati huu huuelezea utakatifu wa Mungu ulio thabiti na huonyesha kwa nini dhambi humkasirisha na haiwezi kusamehewa kwa urahisi:



08FollowYourHeart-Swahili-edited by SB.05.22.56pages.indd 31 27-05-2022 15:05:51

*Lakini Bwana Mwenye Nguvu Zote atatukuzwa kwa ajili ya haki yake, naye Mungu Mtakatifu atajionyesha mwenyewe kuwa mtakatifu kwa haki yake.* (Isaya 5:16)

Na:

*Macho yako ni safi mno hata yasiweze kuutazama uovu, wala huwezi kuvumilia makosa.* (Habakuki 1:13)

**Tabia ya Mungu: Haki na upendo**

Biblia huonyesha kuwa ingawa Mungu ana sifa nyingi (kama zile zilizotajwa kwenye majina 99 ya Mungu kwenye Uislamu), mbili ziko juu sana. Kiasili yeye ni *mwenye haki*, ndicho kipengele cha msingi cha nafsi yake. Matendo na fikra za dhambi hukabiliana na haki hiyo, na kama zinavyoonyesha taarifa nyingi kwenye siku za mwanzo za uhusiano wa Mungu na wanadamu, hukumu za kutisha zinaweza kufuata. Shetani na malaika zake walioanguka walitupwa kwenye mashimo ya majonzi wasisamehewe kamwe wala kukombolewa (2 Petro 2:4), kila mzaliwa wa kwanza wa kiume wa Misri aliuawa katika usiku mmoja kwa sababu ya taifa kumpinga Mungu (Kutoka 12:29), huku Waisraeli wengi wakiangamia jangwani kila walipompinga Musa na kumkataa Bwana (Hesabu 11:33, 16:35).

> Kushikilia kwa nje taratibu za kidini hakuwezi kufidia moyo ulio baridi kwake.

Uadilifu mkuu wa pili kwenye tabia ya Mungu ni *upendo* wake uliofungamana na kina cha nafsi yake kiasi cha Biblia kutamka tu kuwa *Mungu ni upendo* (1 Yohana 4:8). Lakini huku haki yake ikiwa kwenye mstari wa mbele wa nafsi yake na kuwasilishwa upesi kwa wale waliomkataa nyakati zile za mwanzo, upendo wake huonekana ulichukua muda kukua na kuinuka kutoka kwenye maficho ya ndani sana ya nafsi yake. Haukuwa mapenzi ya kawaida tu kwa ajili ya watu wake, bali ulitokana na nia yenye kina ya kuwapatia ustawi bora *bila kujali* uadui wao



08FollowYourHeart-Swahili-edited by SB.05.22.56pages.indd 32 27-05-2022 15:05:51

kwake. Ulikuwa upendo unaozidi kutiwa nguvu kwa ulimwengu ulioendelea kuthibitisha kuwa si wa kupendwa. Kufikia wakati wa Yeremia na Ezekieli upendo wa Mungu ulikuwa umefikia upeo wake, na ingawa Mungu alikuwa na haki ya kuwahukumu wanadamu wote kwa sababu ya uovu wao, alichagua kuonyesha ukamilifu wa upendo wake kwao, akitoa kauli yenye uamuzi na uhakika, iliyoweka msimamo wake kwa wanadamu siku zote zijazo:

> *"Nimekupenda kwa upendo wa milele, nimekuvuta kwa wema."* (Yeremia 31:3)

Baada ya kutafakari kwa kina na kukusudia kwa ndani, aliamua kuendelea, na mara akatamka alivyopanga kuubadilisha kabisa uhusiano huu wa Mungu na wanadamu. Kwa njia hii aliwaleta hawa wawili pamoja, akiwaunganisha kwa uthabiti katika ushirika, ukarimu, kufahamiana kibinafsi na urafiki wa wao kwa wao.

## Moyo mpya

Mungu alitamka:

> *"Siku zinakuja," asema Bwana, "nitakapofanya agano jipya na nyumba ya Israeli na nyumba ya Yuda. Halitafanana na agano nililofanya na baba zao wakati nilipowashika mkono kuwaongoza watoke Misri, kwa sababu walivunja agano langu, ijapokuwa nilikuwa mume kwao," asema Bwana. "Hili ndilo agano nitakalofanya na nyumba ya Israeli baada ya siku zile," asema Bwana. "Nitaweka sheria yangu katika nia zao, na kuiandika mioyoni mwao. Nitakuwa Mungu wao, nao watakuwa watu wangu. Mtu hatamfundisha tena jirani yake, wala mtu kumfundisha ndugu yake akisema, 'Mjue Bwana Mungu,' kwa sababu wote watanijua mimi, tangu aliye mdogo kabisa kwao, hadi aliye mkuu sana," asema Bwana. "Kwa sababu nitasamehe uovu wao, wala sitazikumbuka dhambi zao tena."* (Yeremia 31:31-34)



08FollowYourHeart-Swahili-edited by SB.05.22.56pages.indd 33 27-05-2022 15:05:51

Haijawahi kutokea ahadi kama hii – Mungu kuwapa watu wake msukumo na uweza wa kimungu kutoka ndani yao wazitunze sheria zake takatifu, akiwafungulia mlango watu wake wote ili wamjue kibinafsi, na kutoa hakikisho la kusamehe dhambi zao zote hapa na sasa. Na hili halikutosha. Kupitia nabii Ezekieli Mungu aliendelea:

> *Nitawapa moyo mpya na kuweka roho mpya ndani yenu, nitaondoa ndani yenu moyo wenu wa jiwe na kuwapa moyo wa nyama. Nami nitaweka Roho yangu ndani yenu na kuwafanya ninyi mfuate amri zangu na kuwafanya kuwa waangalifu kuzishika sheria zangu.* (Ezekieli 36:26-27)

Na Mungu akaongeza:

> *... nitawaokoa kutoka dhambi zao zote zilizowarudisha nyuma, nami nitawatakasa. Wao watakuwa watu wangu, nami nitakuwa Mungu wao.* (Ezekieli 37:23)

Tofauti na agano la mwanzo, ambapo Mungu aliwaagiza watu wake kwa nguvu kwamba “mta...” na “hamta...”, akiwawekea wajibu wa kumtii kwa moyo mkunjufu, sasa alitamka kwa nguvu, “nita..., nita..., nita...”. *Hivyo alijiwekea mwenyewe jukumu la kuhakikisha kuwa watu wake watamwitikia kwa uaminifu.* Imani ya kweli ilikuwa imefikia upeo wake. Uaminifu wa Mungu ulikuwa unakwenda hadi mwisho wake – *ukiihakikisha* imani ya wale waliokuwa tayari kuingia kwenye uhusiano naye binafsi wenye kina kwa kupitia kwenye mlango huo aliowafungulia wazi.

### *Kizazi kipya chenye heri*

Bila shaka malaika wa mbinguni walishangaa, ni kwa namna gani Mungu ataupatanisha mwaliko huo wa wazi na haki yake iliyo thabiti ambayo kwa jinsi ilivyo huwatenga mbali wenye dhambi. Haki iliyo kamili itawezaje hatimaye kutoa njia kwa neema na huruma iliyo kamili? Mungu atawezaje kuanzisha nyakati mpya zenye heri ambamo watu wake, ingawa ni wenye



08FollowYourHeart-Swahili-edited by SB.05.22.56pages.indd 34 27-05-2022 15:05:51

dhambi mpaka kiini chao, wangeweza dhambi, wangeweza kusamehewa hivyo hata wakaishi katika uhusiano wenye utakatifu kamili naye na wakamjua kutoka ndani ya nafsi zao? Kwa kifupi, Roho Mtakatifu wa Mungu atawezaje kustarehe ndani ya mioyo ya wanadamu wasio watakatifu? Mungu aliwapa jibu:

> *"Ninakwenda kumleta mtumishi wangu, Tawi … nami nitaiondoa dhambi ya nchi hii **kwa siku moja**."*
>
> (Zekaria 3:8-9)

Mungu alikuwa tayari kuingia kwenye hali mbaya zaidi ya ulimwengu wa kibinadamu iliyojaa giza nene la kiroho.

Kwa karne nyingi Mungu alikuwa akitamani watu wake wamkubali, wawe karibu naye na wayatii maagizo yake kutoka mioyoni mwao. Lakini ukaidi wao ulivyoongezeka, ndivyo upendo wake ulivyoongezeka hadi ukawa siyo tu kutaka ushirika wa karibu nao unaozidi uhusiano wa bwana na mtumishi wake. Mungu alijua kuwa njia pekee ya kuweka daraja kwenye pengo kati ya tabia yake iliyo takatifu sana na uovu wa wanadamu usio na utakatifu, itakuwa kwa yeye mwenyewe kulilipa deni tulilopaswa kulilipa ili kuiridhisha hasira yake na kuithibitisha haki yake. Aliahidi kutuma mkombozi aliyemwita '*Tawi*', wa kuuleta ukombozi kwa wanadamu ndani ya siku moja. Lakini ni wazi kuwa itabidi mkombozi huyu aje *kutoka kwenye asili yake mwenyewe*, ikiwa atailipa kikamilifu hiyo gharama ya juu sana iliyotakiwa kwa kuupata msamaha wa watu wa Mungu, na kulifanya hilo ndani ya masaa machache tu.

### Kusudi kuu la Mungu

Mungu alirudi kwenye ahadi yake kwa Daudi kuwa atampa mwana atakayetawala milele juu ya ufalme wake. Kumbuka Mungu alivyosema:



08FollowYourHeart-Swahili-edited by SB.05.22.56pages.indd 35 27-05-2022 15:05:51

*Nitakuwa baba yake, naye atakuwa mwanangu.*

(2 Samweli 7:14)

Kumbuka pia kilichoonyeshwa hapo mapema kwamba neno hili halitoki kwenye andiko la asili la Kikristo, linapatikana kwenye Maandiko ya Wayahudi yaliyoandikwa karne nyingi kabla ya enzi ya Kikristo. La muhimu hapa ni kuwa Mungu alikuwa tayari kumtoa Mwana wake mwenyewe ili aweze kulifanikisha lengo lake kuu la kuwaacha huru kikamilifu wote watakaomwamini na hivyo kupata msamaha wa dhambi zao, na karama ya bure ya uzima wa milele. Tunachoona hapa ni kusudi kuu la Mungu – kumhusisha mwanadamu kwenye uhusiano wote wa karibu zaidi – na alichokuwa tayari kufanya kuweza kulifanikisha hili. Kwa ufupi, Mungu alikuwa tayari kumtuma Mwanawe mwenyewe kwa ajili ya wokovu wa ulimwengu ili tusiwe tena watumishi wasio na thamani bali tuwe watoto wa Mungu waliokombolewa, na warithi wa ufalme wake wa milele. Mungu alikuwa tayari kuingia kwenye *hili la kumhusisha mwanadamu kwenye uhusiano wa karibu kabisa* ili tuweze kuiona nuru yake yenye utukufu.

Baada ya kupitia uzoefu uliokuwa wenye uchungu kabisa alipokuwa akiamua kuurarua moyo wake ili atukomboe, Mungu alijiruhusu kuwa na muda mfupi wa kufurahia matokeo yake ya baadaye. Kwa furaha kuu na faraja halisi alitamka:

*Watakuwa watu wangu, nami nitakuwa Mungu wao. Nitawapa moyo mmoja na kutenda pamoja, ili kwamba waniche daima kwa mema yao wenyewe na kwa mema ya watoto wao baada yao. Nitafanya nao agano la milele: Kamwe sitaacha kuwatendea mema, nami nitawavuvia kunicha mimi, ili kamwe wasigeukie mbali nami. Nitafurahia kuwatendea mema, na kwa hakika nitawapanda katika nchi hii kwa moyo wangu wote na roho yangu yote.*

(Yeremia 32:38-41)



08FollowYourHeart-Swahili-edited by SB.05.22.56pages.indd 36 27-05-2022 15:05:51

Aliendelea kuuthibitisha msamaha kamili wa dhambi zao zote ili waweze kumjua wao binafsi na waishi kwa furaha kuu kwa sifa na utukufu wake:

*Nitawatakasa dhambi zote walizofanya dhidi yangu, na nitawasamehe dhambi zote za uasi dhidi yangu.*

(Yeremia 33:8)

Hivyo tunakwenda kwenye enzi ya Agano Jipya lenye utukufu aliloahidi Mungu.



08FollowYourHeart-Swahili-edited by SB.05.22.56pages.indd 37 27-05-2022 15:05:51

## YESU KRISTO:
## MWANA WA DAUDI, MWANA WA IBRAHIMU

Ukristo una mtazamo hasi sana kuhusu asili ya wanadamu – yaani wafungwa wa dhambi wanaotumikishwa nayo hata hawawezi kujiweka huru – lakini pia una mtazamo chanya kabisa kuhusu hali watakayoweza kuwa nayo wanaume na wanawake – yaani hali ya kuwa wana na mabinti wa Mungu, waliozaliwa kwa Roho Mtakatifu wake, wakabadilishwa na kuwa katika mfano wake binafsi, na wakiuonyesha utukufu wake milele yote. Hata hivyo, mkombozi mkuu wa Mungu alipokuja kuikamilisha hali hiyo, watu wake mwenyewe hawakumwona na utume wake bado unapuuzwa na kukataliwa na mamilioni mengi ya watu hata leo.

### Kumtarajia Masihi

Maandiko 17 ya kinabii yaliyooandikwa wakati Mungu aliahidi agano jipya yalifikisha kileleni mafunuo ya Mungu kwa Wayahudi. Ahadi ya kuja kwa Masihi, mkombozi, ilipaswa kuwa tumaini lao kuu na la mwisho, maana makusudio ya Mungu kwa ajili ya wanadamu yatatimizwa. Baada ya vitabu hivi kuandikwa hakukuwa na vingine. Kulikuwa na ukimya wa kama miaka 400. Kufikia wakati wa kuzaliwa kwa Yesu, taifa la Israeli lilikuwa na matarajio yenye shauku ya kumwona Masihi. Ahadi za Mungu kwa Ibrahimu hazo zilikuwa zimefuatwa na kipindi kama hicho cha ukimya wa zaidi ya miaka 400, kabla agano la mwanzo halijaanzishwa kupitia kwa Musa. Wakati wa kutolewa agano jipya hakika ulikuwa umefika. Waisraeli walisubiri kwa hamu, na kwa usahihi - maana ni jinsi ilivyotukia - walimtarajia Masihi aonekane wakati huo. Hata hivyo, alipokuja, ni wachache tu waliomtambua, huku taifa kwa ujumla wakimpuuza, na kibaya zaidi, walimpinga na kumkataa.

> Ibrahimu aliiona kimbele Injili nzima.



08FollowYourHeart-Swahili-edited by SB.05.22.56pages.indd 38 27-05-2022 15:05:51

Mungu alimwahidi Daudi mwana atakayetawala milele juu ya ufalme wake. Siku moja Yesu alipowauliza Wayahudi:

*“Mnaonaje kuhusu Kristo? Yeye ni mwana wa nani?” Wakamjibu, “Yeye ni mwana wa Daudi.”* (Mathayo 22:42)

Sulemani mwana wa Daudi, alikuwa mfalme wa Israeli mwenye mafanikio na nguvu zaidi. Katika siku zake, Israeli iliutawala ulimwengu ulioizunguka. Amani ilienea. Sasa taifa lilikuwa likitamani mfalme mpya wa kuanzisha utawala kama huo na ambao hautapita. Walitarajia Masihi-Mfalme wao alifanye taifa la Kiyahudi kuwa la nguvu na tajiri zaidi duniani. Lakini walikosa jambo moja muhimu – na hawakuwa na udhuru kwa kutoliona na kulizingatia. Mungu alikuwa ameshaahidi mwana kwa baba *mwingine* (Ibrahimu) miaka mingi kabla ya wakati wa Daudi na Isaka, na huyo mwana (Isaka) yeye naye alipaswa kuwa mfano wa Mwana mkuu atakayekuja. Hivyo Wayahudi walipaswa kumtilia *huyo* maanani zaidi, kwa sababu Masihi atakuja kwanza kwa jinsi ya mfano wa Isaka kabla hajaja kwa jinsi ya mfano wa Sulemani.

**Mwana wa Ibrahimu**

Hatuhitaji kutafuta sana kwenye Maandiko ya Kikristo (Agano Jipya) kutambua huyo Mwana mkuu alikuwa nani. Soma tu kifungu cha mwanzo cha kitabu chake cha kwanza, Injili ya Mathayo. Andiko la mwanzo la Maandiko yote ya Kikristo linasomeka:

*Habari za ukoo wa Yesu Kristo mwana wa Daudi, mwana wa Abrahamu.* (Mathayo 1:1)

Wangemtarajia kwanza Mwana wa Ibrahimu. Tulimwangalia kwa kirefu mwana aliyeahidiwa na Mungu kwa Ibrahimu, huyo Isaka, mwana wa mke wake, Sara. Ibrahimu alipompeleka hadi mlima Moria akamtoe sadaka, *Isaka akasema, “Moto na kuni zipo, Je, yuko wapi mwana-kondoo kwa ajili ya sadaka ya*



08FollowYourHeart-Swahili-edited by SB.05.22.56pages.indd 39 27-05-2022 15:05:51

*kuteketezwa?"* (Mwanzo 22:7) Ibrahimu alijibu *"Mwanangu, Mungu mwenyewe atajipatia mwana-kondoo kwa ajili ya hiyo sadaka ya kuteketezwa."* (Mwanzo 22:8). Kiebrania cha asili kimekazia zaidi – kwa ufanisi kinabainisha itakavyotukia kikisema, 'Mungu atatoa *kutoka kwake yeye mwenyewe* huyo mwana-kondoo kwa hiyo sadaka ya kuteketezwa.' Kwa maana halisi, Ibrahimu alikuwa akimwambia Isaka, "Mwanangu, wewe ndiwe hiyo sadaka, lakini jipe moyo. Wewe ni mfano tu wa mwingine atakayekuja. Siku moja Mungu atatoa kutoka kwake yeye mwenyewe mwana-kondoo wa kweli kama sadaka."

Yohana Mbatizaji (Yahya kwenye Uislamu), akimtazama Yesu alipokuwa akitembea siku moja, alitangaza: *"Tazama, Mwana-Kondoo wa Mungu aichukuaye dhambi ya ulimwengu!"* (Yohana 1:29), akimtambulisha mwana-kondoo huyo aliyemzungumzia Ibrahimu. Kwenye siku nyingine Yesu mwenyewe aliwaambia Wayahudi waliokuwa wakibishana naye: *"Baba yenu Ibrahamu alishangilia kwamba angaliiona siku yangu, naye akaiona na akafurahi"* (Yohana 8:56). Kweli alikuwa nao wakati ule akilini mwake Ibrahimu aliposem: "Mungu atajipatia mwana-kondoo kwa hiyo sadaka, mwanangu."

Ibrahimu aliiona kimbele Injili nzima. Isaka alizaliwa kwa Roho kwenye mazingira ya kipekee, hivyo Ibrahimu alijua kuwa Mwana wa Mungu naye atazaliwa kipekee (Yesu alizaliwa na mwanamke bikira). Ibrahimu alipanga kumtoa sadaka Isaka, akijua ya kuwa Mwana wa Mungu atatolewa sadaka vile vile. Ibrahimu aliamini kuwa Isaka atafufuliwa kutoka kwa wafu. Kwa kufanya hivyo alikuona kimbele kufufuka kwa Mwana wa Mungu. Si ajabu kuona ikitamkwa kuwa andiko *alitangulia kumtangazia Ibrahamu Injili* (Wagalatia 3:8).

Kila linapoulizwa swali llifuatalo: "Ni zawadi gani iliyo kubwa zaidi aliyowahi kukupa Mungu kuonyesha upendo wake kwako?" baadhi husema "afya yangu", wengine "watoto wangu", au na wengine tena "alijibu maombi yangu akanisaidia nilipopata matatizo ya kutisha." Yote haya ni majibu mazuri,



08FollowYourHeart-Swahili-edited by SB.05.22.56pages.indd 40 27-05-2022 15:05:51

ambayo yanaonyesha wema wa Mungu katika kutupa mahitaji yetu na kutuangalia. Lakini kati ya hayo hakuna lililomgharimia cho chote, wala si ushahidi wa kina cho chote cha upendo moyoni mwake kwa ajili yetu. Lakini ikiwa atamtoa Mwanawe afe kwa ajili yetu ili tuweze kupokea uzima wa milele kama zawadi, tusamehewe dhambi zetu zote, na tuweze kumjua Mungu, *hiyo itazidi zawadi zote ambazo ataweza kutoa kwa sababu itamdai gharama isiyo na kifani.* Na hili ndilo hasa lililotokea Yesu alipokuja duniani! Kama mtume Paulo, mmoja wa wanafunzi wake walio maarufu zaidi, alivyoliweka:

> *Ikiwa Mungu hakumhurumia Mwanawe, bali alimtoa kwa ajili yetu sote, atakosaje basi kutupatia vitu vyote kwa ukarimu pamoja naye?* (Warumi 8:32)

**Hazina kuu ya Mungu**

Hii ilikuwa gharama kuu ambayo Mungu alikuwa tayari kuilipa ili aipate hazina kuu aliyokuwa akiitafuta, yaani, watu waliosafishwa, waliosamehewa, ambamo Roho wake mwenyewe aliye Mtakatifu aweze kukaa kwa starehe. Yesu alipokufa msalabani hasira ya Mungu juu ya dhambi ya ulimwengu iliisha yote. Tatizo hili la 'dhambi kwetu - utakatifu kwake', la dhambi-utakatifu, lililosababisha kiwewe kikubwa sana wakati wa Musa na vizazi vilivyofuata, liliisha. Mlango ulikuwa wazi kwa mambo hayo yote mazuri sana aliyokuwa ameahidi Mungu kupitia Yeremia na Ezekieli kuwa yatatimia.

> Ilikuwa zawadi kubwa zaidi sana aliyoweza kutoa kwa sababu itamdai gharama isiyo na kifani.

Waumini wa kweli wa Kikristo, siyo tu wanamwamini Mungu. Kama wangeamini hivyo tu, hawangekuwa na ujumbe maalumu kwa wenzao wa Kiislamu wanaoabudu Mungu mmoja. Lakini sasa wana ujumbe maalumu sana kwa wote wanaokaa duniani wakiwamo na Waislamu. Yesu Kristo, Mwana wa Mungu,



08FollowYourHeart-Swahili-edited by SB.05.22.56pages.indd 41 27-05-2022 15:05:51

aliyakamilisha matumaini ya waumini wote wa kweli alipoyatoa maisha yake kwa ajili ya ukombozi wao. Habili alitoa sadaka ya damu ya wana-kondoo wake kuashiria tumaini lake katika wokovu wa Mungu utakaokuja. Ibrahimu alikuwa tayari kumtoa sadaka mwanawe aishirikishe damu yake kama kivuli na ishara ya upendo mkuu wa Mungu katika kuwa tayari kufanya hivyo siku moja kwa ajili ya Ibrahimu. Musa aliagiza kila familia ya Kiisraeli kuieneza damu ya mwana-kondoo kwenye vizingiti na miimo ya milango, kuashiria kusulibiwa kwa Mwana wa Mungu atakayekuja kuleta ukombozi wao wa milele.

### Watoto wa Mungu

Kutokana na hayo, ujumbe wetu kwa Waislamu na ulimwengu wote ni huu kwamba Yesu tumepokea wokovu wa Mungu, tumepewa msamaha kamili wa dhambi zetu, tumekuwa watoto wa Mungu, tumempokea Roho wa Mungu, ni warithi wa ufalme wa Mungu, na muhimu zaidi, tumepata kumjua Mungu tukiwa watu wake waliokombolewa na kuokolewa.

Mungu alipozungumza na Musa, uso wa Musa uling'ara, ukiakisi uwepo wa Mungu mbele yake na katikati ya watu wake. Utukufu wa Mungu ulidhihirika kwenye hekalu la kwanza la Wayahudi Sulemani alipoliweka wakfu kwa Mungu, uthibitisho mwingine kuwa Mungu alikuwa katikati ya watu wake kwa namna maalumu kabisa. Lakini Yesu Mwana wa Mungu aliposimama katikati ya watu wake, udhihirisho huo ulifikia kipimo kipya. Alichukua watatu kati ya wanafunzi wake akapanda nao hadi juu ya mlima, na ghafla alibadilishwa mbele yao. *Uso wake ukang'aa kama jua na nguo zake zikawa na weupe wa kuumiza macho* (Mathayo 17:2). Wakati huu uthibitisho wa utukufu uliuzidi sana ule wa wakati wa Musa na wa Sulemani, lakini uliendelea kuzidi. Yesu *mwenyewe* alibadilishwa. Utukufu uling'ara kupitia yeye. Hakuuakisi wala kuutazama, aliutoa kutoka ndani yake yeye mwenyewe katika fahari yenye heshima. Mwana wa Mungu alipochukua namna



08FollowYourHeart-Swahili-edited by SB.05.22.56pages.indd 42 27-05-2022 15:05:51

ya mwanadamu, Mungu na wanadamu waliungana milele. Tutaona hivi karibuni ni kwa jinsi gani, katika umilele, wafuasi wa Yesu nao watazalisha utukufu ule ule kutoka ndani yao wenyewe.

**Kwa mikono iliyokunjuliwa**

Kwenye dini nyingine zote zinazotambua Mungu mmoja mfano wa Mungu unakaribiana. Alizifunua sheria zake, aliagiza utii kutoka kwa watumishi wake, akakunja mikono yake akiangalia na kusubiri aone kitakachofuata. Hii ndiyo Dini ya Kaini inayozaa ibada ya Mungu mmoja ya kidesturi tu bila ya imani ya kweli. Lakini katika kutimiza matumainio ya Habili, Ibrahimu na Musa, ambao Mungu alikubali kuwaita marafiki zake, Mungu aliteremka kutoka kwenye kiti chake cha enzi, akakunjua mikono, akaitandaza juu ya dunia yote, akajinyenyekeza na kuujia ulimwengu wetu, akiilipa gharama iliyo kuu kuonyesha upendo wake wa milele ulio thabiti kwa ajili yetu ili atupe hakikisho la mahali penye utukufu katika ufalme wake wa mbinguni.

Wayahudi walimkosa Mwana wa Ibrahimu. Hawakufahamu kuwa ilibidi Masihi aje kwanza kama mwana wa Ibrahimu, katika unyenyekevu kamili, atolewe sadaka kwa ajili ya ukombozi wetu. Paulo analiweka katika maneno haya:

> *Kuweni na nia ile ile aliyokuwa nayo Kristo Yesu: Yeye, ingawa alikuwa na asili ya Mungu hasa, hakuona kule kuwa sawa na Mungu kuwa kitu cha kushikilia, bali alijifanya si kitu, akachukua hali hasa na mtumwa, naye akazaliwa katika umbo la mwanadamu. Naye akiwa na umbo la mwanadamu, alijinyenyekeza, akatii hata mauti: naam, mauti ya msalaba!* (Wafilipi 2:5-8)

Kuna unabii mwingi kwenye Maandiko ya Wayahudi kuhusu kifo cha Masihi cha kujitoa sadaka. Kwa kiasi kikubwa ulifanywa kupitia Daudi na Isaya karne nyingi kabla ya Yesu kuja. Mwingi



08FollowYourHeart-Swahili-edited by SB.05.22.56pages.indd 43 27-05-2022 15:05:51

ulitabiri kwa kina mazingira ya kifo chake (taz. Zaburi 22:1-21, 69:1-29) huku unabii mwingine ukitangaza kusudi la sadaka yake – kuukomboa ulimwengu kutoka kwenye uovu wake – katika lugha dhahiri isiyo na mashaka (taz. Isaya 53:1-12). Manabii hawakukijua kamili kile walichokuwa wakikitabiri, lakini walijua unabii utatimia katika vizazi vijavyo. Kama mtume Petro alivyoliweka:

> *... wale manabii waliosema kuhusu neema ambayo ingewajia ninyi, walitafuta kwa bidii na kwa uangalifu mkubwa, wakijaribu kujua ni wakati upi na katika mazingira gani ambayo Roho wa Kristo aliyekuwa ndani yao alionyesha, alipotabiri kuhusu mateso ya Kristo na utukufu ule ambao ungefuata. Walidhihirishiwa kwamba walikuwa hawajihudumii wao wenyewe, bali waliwahudumia ninyi, waliponena kuhusu mambo hayo, ambayo sasa yamehubiriwa kwenu na wale waliowahubiria ninyi Injili kwa Roho Mtakatifu aliyetumwa kutoka mbinguni. Hata malaika wanatamani kuyafahamu mambo haya.*
>
> (1 Petro 1:10-12)

**Utawala wake katika utukuf*u***

Utabiri mwingi wa utawala wake katika utukufu kama Mwana wa Daudi ambao bado haujaja, nao hujaza kurasa za maandiko yale yale. Wakati mwingine utabiri wa kuja kwa Masihi akiwa mwana anayeteseka wa Ibrahimu ulikuwa katikati ya utabiri mwingine uliotabiri utukufu wake wa mbinguni, kwa hiyo Wayahudi hawakuwa na udhuru. Hapa kuna mfano hasa:

> *Tazama, mtumishi wangu atatenda kwa hekima; atatukuzwa, na kuinuliwa juu, na kukwezwa sana.* [mwana wa Daudi mwenye utukufu] *Kama walivyokuwa wengi walioshangazwa naye, kwani uso wake ulikuwa umeharibiwa sana zaidi ya mtu yeyote na umbo lake kuharibiwa zaidi ya mfano wa mwanadamu: hivyo atayashangaza mataifa mengi, nao wafalme watafunga*



08FollowYourHeart-Swahili-edited by SB.05.22.56pages.indd 44 27-05-2022 15:05:51

*vinywa vyao kwa sababu yake. Kwa kuwa yale ambayo hawakuambiwa, watayaona, nayo yale wasiyoyasikia, watayafahamu.* (Isaya 52:13-15)

Mungu na wanadamu waliungana milele.

Kwanza Paulo anaonyesha jinsi mwana mkuu wa Ibrahimu, Yesu Kristo, siyo tu alivyojinyenyekeza bali alivyokuwa tayari hata kuaibishwa kwa njia ya kifo cha msalabani. Kisha anahitimisha:

*Kwa hiyo, Mungu alimtukuza juu sana, na kumpa Jina lililo kuu kuliko kila jina, ili kwa Jina la Yesu, kila goti lipigwe, la vitu vya mbinguni, na vya duniani, na vya chini ya nchi, na kila ulimi ukiri ya kwamba YESU KRISTO NI BWANA, kwa utukufu wa Mungu Baba.* (Wafilipi 2:9-11)

Yesu aliwapa wakuu wa Kiyahudi wa wakati wake kila dalili ya yeye ni nani hasa na kuwa kuja kwake kulikuwa kumetabiriwa wazi wazi. Musa aliandika habari zake (taz. Yohana 5:46). *Ibrahimu alishangilia kwamba angaliiona siku* yake (Yohana 8:56). Daudi, akivuviwa na Roho, alimwita Yesu Bwana wake (taz. Mathayo 22:43). Walipaswa kumtambua na kumjua.

### Hakuna upendo kuzidi huu

Usiku wa kuamkia kusulibiwa kwake, Yesu alijitambulisha kwa namna nyingine alipowaambia wanafunzi wake:

*"Hakuna mtu mwenye upendo mkuu kuliko huu, mtu kuutoa uhai wake kwa ajili ya rafiki zake. Ninyi ni rafiki zangu mkifanya ninayowaamuru. Siwaiti ninyi watumishi tena, kwa sababu watumishi hawajui bwana wao analofanya, bali nimewaita ninyi rafiki, kwa maana nimewajulisha mambo yote niliyoyasikia kutoka kwa Baba yangu."*

(Yohana 15:13-15)



08FollowYourHeart-Swahili-edited by SB.05.22.56pages.indd 45 27-05-2022 15:05:51

Mfuatano wa Mungu kuwa na uhusiano wa karibu na wanadamu ulikuwa umekamilika. Alimwita Ibrahimu kuwa ni rafiki yake. Alisema uso kwa uso na Musa kama mtu azungumzavyo na rafiki yake. Hivyo sasa Yesu aliweza kuzungumza na wanafunzi wake wote aliokuwa nao kama marafiki wa kweli wa Mungu. Hatimaye mlango ulitaka kufunguka kwa watu wote wa Mungu. Kufa na kufufuka kwa Yesu kulikokaribia kutawafungulia kumjua Mungu wao binafsi, kusamehewa dhambi zao, kumpenda kwa mioyo yao yote, na hatimaye kutukuzwa kwenye kiwango chake yeye mwenyewe. Ndicho Mungu alichokuwa amekitamani kwa shauku kubwa, na ilikuwa kwa ajili ya hicho alikuwa amevumilia mengi sana.

## ROHO MTAKATIFU: UWEPO WA MUNGU KUKAA NDANI YETU

Baada ya Yesu kufufuka katika wafu aliwatokea wanafunzi wake nyakati tofauti. Siku ya arobaini alipaa mbinguni baada ya kuwaambia: *"Tazama nitawatumia ahadi ya Baba yangu; lakini kaeni humu mjini hadi mtakapovikwa uwezo utokao juu"* (Luka 24:49). Aliutambulisha wazi wazi uwezo huo: *"... baada ya siku chache mtabatizwa kwa Roho Mtakatifu"* (Matendo 1:5). Siku kumi baada ya kupaa kwake, wanafunzi walipokuwa wamekusanyika mjini Yerusalemu, *ghafula sauti kama mvumo mkubwa wa upepo mkali uliotoka mbinguni* na ghafla *wote wakajazwa na Roho Mtakatifu* (Matendo 2:2-4).

### Nia kuu ya Mungu

Nia kuu ya Mungu ya kuingia kwenye uhusiano wa karibu kabisa na watu wake, ilitimizwa Roho wake mwenyewe aliposhuka juu ya wanafunzi wa Yesu. Ulikuwa mwanzo wa enzi ya agano jipya la heri. Mungu na mwanadamu waliungana – kwa milele yote! Kilele cha lengo lake kuu kilikuwa kimefikiwa. Wakati Yesu Mwana wa Mungu akiwa kati ya Waisraeli katika namna ya mwanadamu, Mungu alikuwa *pamoja* na watu



08FollowYourHeart-Swahili-edited by SB.05.22.56pages.indd 46 27-05-2022 15:05:51

wake katika namna ya kibinadamu yenye nguvu na ukaribu kuliko ilivyowahi kutokea wakati wa Musa. Lakini sasa, Roho Mtakatifu alipokuja kuishi katika mioyo ya watu wa Mungu na kubaki humo hadi Yesu atakaporudi, Mungu akawa yupo *ndani ya* watu wake, akikaa kwenye maficho ya ndani sana ya mioyo yao.

Kumbuka hili:

Waumini wa kweli wa Kikristo, waliozaliwa kwa Roho wa Mungu, humjua Mungu kibinafsi.

Humruhusu Roho wake kuichunguza kwa kina mioyo yao, kung'oa kila kutoamini, majivuno, kiburi, tamaa, kujiridhisha kidini, na uovu.

Wana hakikisho kamili la uzima wa milele.

Wanajua kuwa dhambi zao zote zimesamehewa.

Wanampenda Bwana kwa mioyo yao yote.

Wanajua kuwa Mungu anastahili upendo wao wa ndani kabisa, akiisha kulipa gharama ya thamani sana ili awakomboe.

Wakiutazama upendo huo, uliokamilishwa katika sadaka ya Mwanawe, wako huru kumpenda kwa mioyo yao yote, na kwa nafsi na akili zao zote.

Hakuna kinachowatenganisha na ufalme wa mbinguni.

**Kumjua Mungu kibinafsi**

Mtume Paulo aliwahubiri waumini wa kweli wa kwanza wa Kikristo hivi: L*akini sasa kwa kuwa mmemjua Mungu, au zaidi mmejulikana na Mungu* (Wagalatia 4:9). Hili huonyesha wazi kuwa yalikuwa mapenzi mema ya Mungu kuufungua mlango ili ajulikane, si juhudi fulani za kidini kwa upande wa *mwanadamu* zilizomleta kwenye nafasi hii. Na wewe binafsi unaweza kumjua Mungu – kama uko tayari kujikabidhi kwa Yesu Kristo ukapokea ukamilifu wa wokovu wake.



08FollowYourHeart-Swahili-edited by SB.05.22.56pages.indd 47 27-05-2022 15:05:51

Imani ya Ibrahimu, iliyokamilishwa katika utayari wake wa kumtoa sadaka mwanawe, ilikuwa akisi njema ya uaminifu wa Mungu mwenyewe. Lakini zawadi ya Mungu ya Mwanawe kama sadaka kwa ukombozi wetu, ni uthibitisho kamili wa upendo wake wenye nguvu kwa ajili yetu.

> *Hivi ndivyo Mungu alivyoonyesha pendo lake kwetu: Mungu alimtuma Mwanawe wa pekee ulimwenguni, ili tupate uzima kupitia kwake. Hili ndilo pendo: si kwamba tulimpenda Mungu, bali yeye alitupenda, akamtuma Mwanawe, ili yeye awe dhabihu ya upatanisho kwa ajili ya dhambi zetu.* (1 Yohana 4: 9-10)

**Dini ya pekee ya kweli Duniani**

Yesu alisema, *"hakuna mtu anayeweza kuuona Ufalme wa Mungu kama hajazaliwa mara ya pili"* (Yohana 3:3). Hapa tunajumuishwa sote, wewe pia. Mtu kuzaliwa upya kwa Roho wa Mungu ndiyo njia pekee kwake, wakati wo wote, katika umri wo wote, ili awe huru kutoka dhambini mwake na kuwa raia wa mbinguni.

Kurani hukaribia kwa namna ya kuvutia kuukubali ufunuo huu.

Imani ya kweli, ile ya Habili, ndiyo dini ya pekee ya kweli duniani, kama kwa nadra inaweza kuitwa kuwa ni dini. Hasa ni imani iliyo *hai*, na itikio kwa *uaminifu* wa Mungu uliofunuliwa mara ya mwisho kikamilifu katika wokovu wake kwa njia ya Yesu Kristo. Akirejea kwenye tamko la Mungu kuwa Ibrahimu alikuwa mwenye haki machoni pake kwa sababu tu aliuamini uaminifu wa Mungu, Paulo anasema:

> *Maneno haya "ilihesabiwa kwake kuwa haki," hayakuandikwa kwa ajili yake peke yake, bali kwa ajili yetu sisi pia ambao Mungu atatupa haki, sisi tunaomwamini yeye aliyemfufua Yesu Bwana wetu kutoka kwa wafu. Alitolewa afe kwa ajili ya dhambi zetu, naye alifufuliwa kutoka mauti ili tuhesabiwe haki.* (Warumi 4:23-25)



08FollowYourHeart-Swahili-edited by SB.05.22.56pages.indd 48 27-05-2022 15:05:51

Paulo anaendelea: *Kwa hiyo kama mtu akiwa ndani ya Kristo, amekuwa kiumbe kipya; ya kale yamepita, tazama, yamekuwa mapya* (2 Wakorintho 5:17). Watu wa kweli wa Mungu ni wale waliomwamini Yesu, Mwana wa Mungu, na wakapokea ahadi yake kuu, Roho wa Mungu. Wakristo wanaoisoma Kurani huguswa na kauli zake zinazolithibitisha hili. Kurani hukaribia kwa namna ya kuvutia kuukubali ufunuo huu. Kwanza, inasema kuwa malaika alimtokea mama wa Yesu na kumwambia: 'Ewe Maryamu! Mwenyezi Mungu anakupa khabari njema za Neno tu litokalo Kwake. Jina lake ni Masih, Isa, mwana wa Maryamu' (Surah 3:45). Kwenye Kiarabu asilia maneno ya msingi ni 'kalimatim-minhu' 'neno litokalo kwake.' Neno 'minhu' – 'kutoka kwake' – lina maana kuwa Yesu alikuja kutoka kwa Mungu *mwenyewe* na hakuwa tu mwanadamu mwingine wa kawaida.

Kwenye kifungu kingine Kurani inazungumzia waumini wa kweli, 'Hao ndio ambao Ameandika nyoyoni mwao imani na Akawatia nguvu kwa Roho itokayo Kwake' (Surah 58:22). Maneno ya msingi hapa yanafanana sana: 'Roho itokayo Kwake' – 'ruhim-minhu'. Ni ajabu sana kuiona Kurani ikithibitisha kiini cha Injili ya Kikristo. Yesu ndiye Neno aliyetoka kwa Mungu (minhu – 'kutoka Kwake'), na Roho Mtakatifu aliyefuata, naye pia ndiye Roho aliyetoka kwa Mungu ('minhu' – 'kutoka Kwake'). Kurani hukazia kuwa nafsi hizi mbili zilitoka kwa Mungu mwenyewe. Haiutumii msemo huu (minhu) kwa nafsi nyingine yo yote katika muktadha kama huo.

### Mlango uko wazi

Wewe umefunguliwa mlango ili umwamini Mkombozi wa Mungu, Yesu Kristo, na uingie kwenye uhusiano wa binafsi naye kwa kumpokea Roho Mtakatifu. Unahitajika tu kufanya kitu kimoja muhimu cha imani ya kujikabidhi – kumwamini Yesu kama Bwana na Mwokozi wako.



08FollowYourHeart-Swahili-edited by SB.05.22.56pages.indd 49 27-05-2022 15:05:51

Miaka ya hivi karibuni mara nyingi nimewauliza Waislamu maswali matatu muhimu sana. Kwanza, *Wewe binafsi unamjua Mungu?* Umo kwenye uhusiano unaozidi mahusiano yote – uhusiano binafsi na Mungu ulio hai? Pili, *Dhambi zako zimesamehewa kwa sababu ya yeye?* Umesafishwa siyo tu hatia ya dhambi zako zote bali pia nguvu yake? Mwisho, *Unampenda Mungu kwa moyo wako wote, kwa nafsi yako yote, akili zako zote, na nguvu zako zote?* Una ushahidi halisi kuwa kweli Mungu ni wa kupendwa, kuwa amefanya jambo lililo dhahiri kudhihirisha upendo wake kwako, na anataka tu umkubali kwa kumpenda kutoka moyoni?

Nimepokea majibu tofauti kwenye maswali haya, lakini hivi karibuni kijana Mwislamu wa kike alinipa majibu matatu ambayo, kwa mtazamo wangu, huakisi kwa usahihi majibu pekee halisi anayoweza Mwislamu kuyatoa kulingana na theolojia ya Kiislamu. Kwanza, alisema: "Kulingana na Uislamu haiwezekani kumjua Mungu kibinafsi. Unaweza kumwamini na kumwomba na kumwabudu Allah, lakini kamwe huwezi kumjua." Kisha aliendelea: "Vile vile haiwezekani kujua kuwa umesamehewa dhambi zako zote. Unaweza kuomba msamaha, ukajaribu kushika sheria za Allah, na kutumaini rehema zake, lakini kamwe huwezi kujua hakika katika maisha haya kuwa umesamehewa." Mwisho alisema: "Ninampenda Mungu kwa moyo wangu wote? Kamwe sijafikiria hasa kuhusu hilo. Ninamwamini, niko tayari kumtumikia – lakini kumpenda? Kamwe hilo sijalifikiria."

**Habari njema kwa ajili yako**

Habari njema ni kuwa yote matatu yako wazi kwako kujibu. Mungu wa kweli alivivunja vizuizi kati yake na wote wenye dhambi Yesu Kristo alipokufa kwa ajili ya dhambi za ulimwengu. Mlango wa kumpokea Roho wake Mtakatifu na kuishi kwa imani pekee katika yeye (imani ya Habili) ulifunguliwa kwa waumini wote wa kweli, ili wamtegemee kuliko kujaribu bure kujisifu



08FollowYourHeart-Swahili-edited by SB.05.22.56pages.indd 50 27-05-2022 15:05:51

kwake kwa utii wa kitumwa kwenye tmazoea ya kidini na taratibu za ibada zisizobadilika (dini ya Kaini). *Unaweza* kabisa kumjua Mungu, *unaweza* kusamehewa dhambi zako zote, na *unaweza* kumpenda kwa moyo wako wote, kwa nafsi yako yote na kwa akili zako zote. Hizi ndizo funguo za uzima wa milele.

Imani ya Ibrahimu iliakisi uaminifu wa Mungu. Iliangaza kama mwezi ikiurudisha mwanga wa jua. Lakini waumini wa kweli wanaweza kufanya zaidi ya hili. Wanaweza kuuzalisha upendo kwa Mungu wakimpenda Yeye aliwapenda kwanza. Wataangaza kama vijua vidogo katika ufalme wa mbinguni. Yesu alisema: *"Ndipo wenye haki watang'aa kama jua katika Ufalme wa Baba yao"* (Mathayo 13:43). Malaika wataendelea kuuakisi utukufu wa Mungu siku hiyo itakapokuja, lakini waumini wa kweli wa Kikristo watauzalisha wakimrudishia utukufu. Malaika ni watumishi wa Mungu wa mbinguni, lakini watu wa Mungu waliokombolewa duniani ni *watoto* wake wa kiume na wa kike. Wataudhihirisha uwepo wenyewe wa Roho Mtakatifu ndani yao. Nuru yao itaangaza kutoka ndani mwao katika utukufu halisi wa kuonekana. Si ajabu Paulo anapoandika juu ya:

> Waumini wa kweli wanaweza kuuzalisha upendo kwa Mungu wakimpenda Yeye aliyewapenda kwanza.

> *"Hakuna jicho limepata kuona, wala sikio limepata kusikia, wala hayakuingia moyoni wowote, yale Mungu amewaandalia wale wampendao."*
>
> (1 Wakorintho 2:9)

Kwa imani katika Kristo, na kwa imani hiyo pekee, unaweza kuwa mtoto wa kweli wa Mungu, unaweza kumjua Mungu mwenyewe, unaweza kusamehewa dhambi zako zote, na kuwa mrithi wa uzima wa milele. Yesu alisema:

> *"Mimi ndimi njia na kweli na uzima. Mtu hawezi kuja kwa Baba isipokuwa kwa kupitia kwangu."* (Yohana 14:6)



08FollowYourHeart-Swahili-edited by SB.05.22.56pages.indd 51 27-05-2022 15:05:51

Waumini wote wa kweli wa Kikristo wamehakikishiwa:

> *Ingawa hamjamwona, mnampenda; tena ingawa sasa hammwoni, mnamwamini na kujawa na furaha isiyoneneka yenye utukufu usioelezeka. Maana mnaupokea wokovu wa roho zenu, ambao ndio lengo la imani yenu.* (1 Petro 1:8-9)

Mlango uko wazi kwa wanadamu wote duniani, bila kujali habari za maisha yao zikoje bila kujali dhambi zao zilikuwa mbaya kiasi gani mlango uko wazi wa kupokea rehema kamili ya Mungu kwenye enzi hii ya neema na kuwa warithi wa ufalme wake wa milele.

Kama alivyoliweka Yesu:

> *Mimi ndimi lango, yeyote anayeingia zizini kwa kupitia kwangu ataokoka, ataingia na kutoka, naye atapata malisho.* (Yohana 10:9)

Mlango ule utabaki wazi hadi atakaporudi.

*Unabaki wazi kwa ajili yako.*



08FollowYourHeart-Swahili-edited by SB.05.22.56pages.indd 52 27-05-2022 15:05:51

***Maswali***

Maswali yafuatayo yatakuwa na faida kubwa kwa kuufahamu zaidi ujumbe wa kijitabu hiki. Tafadhali tuma majibu yako na utujulishe ni kijitabu kipi kingine utakachopenda kukipokea kutoka kwenye mfuatano wa vijitabu hapa chini.

1. Elezea Uislamu unavyotarajia kwa wafuasi wake kutimiza desturi za dini.
2. Habili alionyeshaje imani ya kweli kwa Mungu?
3. Ikamilishe sentensi: "Ibrahimu akamwamini BWANA; naye kwake ………… …………………………………… ……. ………. "
4. Eleza tofauti ya msingi kati ya jua na mwezi.
5. Toa mfano wa jinsi Mungu alivyomsikiliza Ibrahimu.
6. Musa aliuakisi vipi utukufu wa Mungu?
7. Ikamilishe sentensi: "dhabihu za Mungu ni roho iliyovunjika; … ………… ……… …………… ……………………… ……………… ………" Eleza kwa maneno yako mwenyewe hili lina maana gani kwako.
8. Ni vingapi kati ya vitabu 39 vya Maandiko ya Wayahudi, ambayo yanajulikana kama Agano la Kale katika Biblia, wakati wa manabii Yeremia na Ezekieli?
9. Ilibidi Yohana Mbatizaji (Yahya) aseme nini kuhusu Yesu kinachoelezea kazi yake maalumu?
10. Una jibu gani kwa swali lifuatalo: Ni zawadi gani aliyowahi kukupa Mungu iliyokuwa na thamani zaidi? Ni zawadi gani iliyomgharimu kuliko zote?
11. Elezea kwa kifupi tofauti: "Malaika ni ……………… …… ………………… ……. …………………, lakini watu wa Mungu waliokombolewa duniani ni ………….. ………… ………… …… ……. …………. ………………………"



08FollowYourHeart-Swahili-edited by SB.05.22.56pages.indd 53 27-05-2022 15:05:51

**Vijitabu vilivyopendekezwa kwa ajili ya wasomaji wetu:**

1. Umeumbwa kwa Kusudi
2. Jitahidi Kulinganisha
3. Mwisho Usiojulikana
4. Mpendwa Abdallah
5. Mtu Mwenye Ujumbe
6. Kwa nini Kuiamini Biblia
7. Kurani na Biblia
8. Fuata Moyo Wako

Al-Kitab - Kitabu cha Vitabu (kozi ya Biblia kwa njia ya posta)

*Tafadhali nitumie* ....................................................................

..........................................................................................

..........................................................................................

..........................................................................................

Tuma barua yako kwa:

Hamasa ya Milele
S.L.P. 11795
Arusha, TANZANIA
hymilele@gmail.com

Life Challenge
P.O. Box 50770 - 00200
Nairobi, KENYA
info@life-challenge.org



08FollowYourHeart-Swahili-edited by SB.05.22.56pages.indd 54 27-05-2022 15:05:51

08FollowYourHeart-Swahili-edited by SB.05.22.56pages.indd 55 27-05-2022 15:05:51

08FollowYourHeart-Swahili-edited by SB.05.22.56pages.indd 56 27-05-2022 15:05:51